Jumamosi Desemba 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581602
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com




TEN HAG: ONANA BADO NAMBA MOJA

UKURASA 22

# Matokeo utafiti VVU yaonyesha mafanikio

• **Maambukizi** kwa vijana yapungua, rushwa ngono bado kikwazo... *Endelea ukurasa 3*




UKURASA WA 2

**Mstaafu** jela kwa kumhonga ofisa utumishi



UKURASA WA 10

**Sheria** Mahakama ya Kadhi yafutwa



UKURASA WA 17

**Mapigano** makali yazidi kutikisa Ukanda wa Gaza



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Falme za Kiarabu na Mtawala wa Abu Dhabi, Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan (kulia) na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres wakati wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) katika Jiji la Dubai jana. **PICHA: IKULU**

## Jaji Mkuu akerwa na mawakili kutumia lugha chafu

UKURASA 2

## Samia aeleza maumivu nchi mabadiliko ya tabianchi

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, YANGA SC FANYENI KWELI UK.24
**KATUNI** UK.6

# Rais aeleza maumivu mabadiliko tabianchi

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Tanzania inapoteza asilimia mbili hadi tatu ya Pato la Taifa (GDP) kutokana na mabadiliko ya tabianchi huku akizitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi zao katika kukabiliana na tatizo hilo.

Samia aliyasema hayo jana katika mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), unaoendelea Dubai katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Mkutano huo umehusisha zaidi ya washiriki 70,000 kutoka nchi 190 ambao wamekutana kuzungumzia mabadiliko ya tabianchi duniani. Mkutano huo ulianza Novemba 30 na utaendelea hadi Desemba 12, mwaka huu.

Rais Samia alitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi zao mbalimbali kuhusu kuzisaidia nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kutoa Dola za Kimarekani bilioni 100 kila mwaka.

Alisema walikubaliana kutoa fedha hizo kuzisaidia nchi masikini lakini kiasi kilichotakiwa hakijafikiwa, hivyo ni vizuri ahadi hizo zikatekelezwa ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Walikubaliana kushusha hali ya joto kuhakikisha haivuki nyuzi joto moja. Hali hiyo imekuwa tofauti na imekuwa na matokeo hasi katika nchi za Afrika.

"Kwa mfano kwa Tanzania tunapoteza asilimia mbili hadi tatu ya pato la taifa kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Licha ya Tanzania kuchangia kidogo kwenye ongezeko la joto dunia, imekuwa ikihamasisha uungwaji mkono kwenye kuongeza matumizi ya nishati safi na yenye bei rahisi," alisema Rais Samia.

Alisema jambo la mabadiliko ya tabianchi sio jambo la kuchagua bali ni dharura ambayo inataka nchi zote kushiriki.

"Ripoti ya hivi karibuni ya kisayansi ya dunia inasema jitihada zilizopo sasa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi huenda zikazidiwa, hivyo inahitajika kuongeza juhudi kwa kuwa jambo hili ni kuongeza juhudi la sivyo tufuate sayansi au kupigwa na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi,"alisema Rais Samia.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Ikulu, iliyotolewa awali, Tanzania inaunga mkono hoja ya kuongeza fedha za ufadhili kwa kuzingatia athari zinazozidi kuongezeka kwa sasa na kuhakikisha ahadi ya nchi zilizoendelea kutoa Dola bilioni 100 kila mwaka kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinatimizwa.

Pia kuhakikisha mkutano unaridhia uanzishwaji wa mfuko wa kupambana na majanga na maafa yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha juhudi za matumizi ya nishati safi zinakuwa jumuishi na kujikita pia katika nishati safi za kupikia kwa akina mama vijijini kama njia ya kuhimiza nishati za mpito zinazozingatia usawa wa kijinsia.

"Kuhakikisha mjadala wa masuala ya jinsia unazingatia maadili ya kitaifa na kijamii na wanawake wanapewa kipaumbele katika hatua za kushugulikia mabadiliko ya tabianchi," ilisema taarifa ya Ikulu.

Taarifa hiyo ilisema ujumbe wa Tanzania utashirikisha mawaziri, makatibu wakuu, mabalozi, viongozi na wataalamu kutoka wizara za kisekta, idara za serikali, mashirika ya umma, vyuo vikuu, sekta binafsi, asasi za kiraia, vijana na waandishi wa habari kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Kaulimbiu ya mkutano huo ni, "UNITE. ACT. DELIVER". Kitaifa kaulimbiu ni "Kuimarisha Kilimo Himilivu na Uchumi wa Bluu katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi."

Lengo la kaulimbiu ni kutoa msisitizo katika matumizi ya teknolojia na mbinu bora zinazozingatia changamoto za mabadiliko ya tabianchi, ili kuongeza tija katika uzalishaji, mnyororo wa thamani wa mazao na masoko.



Jaji Mkuu wa Tanzania, Ibrahim Juma, akizungumza wakati wa sherehe ya 69 ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili 279 wapya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Jaji Mkuu akerwa na mawakili kutumia lugha zisizo na maadili

**Na Kulwa Mzee**

JAJI Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, amesema amepokea malalamiko kutoka kwa majaji kuhusu mawakili wa kujitegemea kutumia lugha zinazokiuka maadili ndani ya mahakama.

Kutokana na hali hiyo, amekitaka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kuchukua hatua kabla ya majaji kulalamika.

Prof. Juma alibainisha hayo jana katika hafla ya kuwakubali na kuwatunuku vyeti mawakili wapya 279. Kati ya mawakili hao wapya, wanawake ni 118 na wanaume 161.

Alisema nasaha zake kwa mawakili hao anazielekeza katika maeneo matano, ambayo ni maadili, wajibu wao kwa mahakama na jamii, nani wanafaa kuwaiga kufanya kazi, uwezo na tahadhari.

"Kila mwaka tunazungumzia maadili, asilimia 99 ya kazi za uwakili zinategemea maadili. Tukiififisha mahakama tunafifisha taaluma. Ukikubaliwa kuwa wakili unachukuliwa kuwa una uwezo.

"Uwezo ukitoweka unaingia katika hatua ya kuvunja maadili, tuwe waangalifu katika eneo la maadili, kwani linachafua taswira yote ya sheria," alisema Jaji Mkuu.

Alisema uwakili ni taaluma yenye heshima, vitendo, kauli, saini na mihuri vyote vinatakiwa kuwa na heshima.

"Kila taaluma duniani inategemewa itajidhibiti na kuwadhibiti wanachama wake. TLS ikifanya hivyo hakuna mtu wa kuwaingilia, tofauti sasa chombo kikichukua hatua mawakili wanakusanyika kutetea.

"Sasa chama chenyewe kichukue hatua za kinidhamu, tumieni mamlaka mliyonayo kujidhibiti wenyewe, tumieni kanuni zenu za uwakili za mwaka 2022 kujidhibiti ni wajibu kuonyesha nidhamu kwa mahakama," alisisitiza.

Prof. Juma alisema amepokea malalamiko kadhaa kutoka kwa majaji kuhusu lugha zinazotumika mahakamani na mawakili na kwamba majaji wanatumia busara kwa kuwa zinakiuka Kanuni ya 92 ya Maadili ya Mawakili.

"Wakili ukijibizana na majaji au hakimu unakiuka kanuni zenu. Ikitokea tukio kama hilo isiwe hadi jaji alalamike, mawakili wachukue hatua likitokea kwa kumchukua wakili husika na kumfikisha kwenye vyombo na kutoa adhabu, "alisema Jaji Mkuu.

Kabla ya kuzungumza hayo aliwakubali na kuwatunuku vyeti mawakili hao 279.

"Kwa mamlaka niliyopewa na Sheria ya mawakili sura ya 341 Toleo la 2019, kifungu cha 8(3) nina tamka kwamba wale wote ambao majina yao yamesomwa hapa wamekubaliwa kuwa mawakili na wameorodheshwa rasmi kwenye orodha ya mawakili kuanzia leo Desemba Mosi," alitamka Jaji Mkuu.

Alisema idadi hiyo ya mawakili wapya inafanya jumla ya mawakili sasa kufika 11,916 kutoka idadi ya awali ya mawakili 11,636.

## Mstaafu jela kwa kumhonga ofisa utumishi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, imemhukumu Jesca Yegera (60) mkazi wa Mtaa wa Mwanzugi, Kata ya Igunga Mjini na mwalimu mstaafu wa Shule ya Msingi Mwanzugi, kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela.

Mstaafu huyo amehukumiwa kifungo hicho baada ya kukutwa na hatia katika makosa mawili ya kushawishi na kutoa rushwa ya Sh.500,000 kwa ofisa utumishi.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, Mazengo Joseph, aliiambia mahakama hiyo mbele ya Hakimu Edda Kahindi kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Juni24, 2022.

Alidai katika tarehe hiyo, majira ya mchana, akiwa kwenye ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, mshtakiwa alimshawishi kumpatia rushwa ya sh. 500,000 kwa njia ya simu Ofisa Utumishi Mwandamizi Erick Sije (38) wa halmashauri hiyo.

Aliendelea kudai kuwa mshitakiwa huyo alitoa rushwa ya Sh. 300,000 kati ya Sh. 500,000 alizoahidi kwa njia ya simu ili amsaidie kupata madai yake ya malimbikizo ya mishahara ya miezi mitano aliyokuwa anadai toka serikalini ambayo ni Sh. 6,175,000.

Joseph alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo mawili kinyume cha kifungu namba 15 (1) (b) (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329 mapitio ya mwaka 2019.

Baada ya kusomewa mashitaka hayo mawili, mshitakiwa alikana na upande wa mashitaka kupeleka mashahidi sita mahakamani hapo. Upande wa mshtakiwa ulikuwa na mashahidi wawili yeye na mume wake ambao pia waliwasilisha ushahidi wao mbele ya hakimu huyo.

Hakimu Edda baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, alijiridhisha bila kuacha shaka na ushahidi wa upande wa Jamhuri na kumtia hatiani mshtakiwa.

Aidha Mahakama hiyo ilimhukumu Jesca kutumikia kifungo cha miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. milioni moja ili kuwa fundisho kwa watu wengine.

Hata hivyo hadi mwandishi wa habari hii anaondoka mahakamani hapo, Yegera alikuwa bado hajalipa faini huku akiendelea kubaki chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi.

SIKU YA UKIMWI

# Rushwa ngono bado kikwazo

**Na Rose Jacob,** UKEREWE

RUSHWA ya ngono inayoendekezwa katika kambi za wavuvi katika visiwa mbalimbali wilayani Ukerewe, imetajwa kuwa chanzo cha kuongezeka kwa maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) na kuzorotesha vita dhidi ya VVU na Ukimwi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Bomboka, alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani huku akisema wavuvi wamekuwa wakitoa ajira kwa kinamama wa kupika chakula na shughuli mbalimbali katika kambi zao kwa kutaka rushwa ya ngono.

"Tunapaswa kupiga vita ukatili wa kingono kwani kumekuwapo na shida ya watu wenye virusi vya Ukimwi kufanya ukatili wa kijinsia kwa kuwabaka watoto, kuwalawiti na kuwaambukiza VVU kwa makusudi. Tunaomba tabia hii isijitokeze hapa Ukerewe," alisema Bomboka.

Pia aliwataka watumishi na wananchi wilayani hapa kuhakikisha elimu ya masuala ya Ukimwi inakuwa endelevu na tohara ya kitabibu kwa wanaume izingatiwe ili kupunguza maambukizi mapya.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa shughuli za VVU/Ukimwi kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, 2023 katika Wilaya ya Ukerewe, Mratibu wa Ukimwi wilayani hapa, Anord Mafuru, alisema utoaji wa dawa za kufubaza virusi ARV na za kutibu magonjwa nyemelezi unaendelea.

"Hadi Septemba 2023, Watu Waishio na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) 13,583, wakiwamo wanaume 4,827 na wanawake 8,756 wanatumia ARV na waliopima ni 22,874 kati ya hao waliokutwa na maambukuzi ni 1,960 wanawake wakiwa 1,195 na wanaume 765," alisema Mafuru.

Mjumbe wa Watu Waishio na Virusi vya Ukimwi (WAVIU), Elizabeth Nagagwa, alisema wanakabiliwa na tatizo la huduma za matibabu hususani uchomwaji wa sindano kutokuwa na elimu ya bima ya afya hali inayosababisha kukosa huduma stahiki.




Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Asha Ressa Izina akikata utepe kuzindua gari jipya la wagonjwa la taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Utafiti mpya VVU waonyesha mafanikio

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua matokeo ya awali ya Utafiti wa Viashiria vya Matokeo ya Ukimwi Tanzania kwa mwaka 2022/23 ambayo yanaonyesha kiwango cha ushamiri wa maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) kwa watu wenye umri wa miaka 15 yanaendelea kupungua.

Matokeo hayo yanaonyesha miongoni mwa watu wazima wenye umri wa miaka 15, maambukizi hayo yanaendelea kupungua kutoka watu 72,000 waliokuwapo mwaka 2016/17 hadi watu 60,000 kwa mwaka 2022/23.

Akizindua ripoti hiyo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Morogoro, Majaliwa alisema kwa sasa nchini maambukizi kwa watu wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ni asilimia 4.4.

Alisema katika matokeo ya awali ya utafiti huo, Tanzania Bara ni asilimia 4.5 na kwa Zanzibar 0.4 na kwa jinsia ya wanawake kiwango cha maambukizi ni asilimia 5.6 kulinganisha na wanaume asilimia 3.0.

"Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 0.18 ambapo asilimia 0.24 ni wanawake na asilimia 0.11 ni wanaume. Kwa hiyo wanaume ni wachache kwa sababu hawajitokezi kupima," alisema.

Alisema utafiti umebaini kiwango cha kufubaza VVU kinaendelea kukua kwa wastani wa asilimia 78. Kwa wanawake kiwango kimekuwa kwa asilimia 80.9 na wanaume asilimia 72.2 ukilinganishwa na asilimia 52 iliyokuwapo kulingana na utafiti wa mwaka 2016/17.

Kuhusu ushamiri wa VVU kwa umri wa kuanzia miaka 15 na zaidi kwa mikoa ya Tanzania Bara ,Waziri Mkuu alisema utafiti umeonyesha kinaanzia asilimia 1.7 kwa mkoa wa Kigoma hadi kufikia asilimia 12.7 kwa mikoa ya Njombe, Mbeya na Iringa.

"Mkoa wa Njombe una viwango vya ushamiri zaidi ya asilimia tisa sawa na mara mbili ya kiwango cha taifa na upande wa Zanzibar yanaonyesha unaanzia asilimia 0.2 katika mkoa wa Kaskazini Pemba hadi asilimia 0.8 mkoa wa Kusini Unguja.

"Kiashiria hiki ni muhimu kwa sababu mtu anapokuwa amefubaza VVU anakuwa na afya njema na hatosumbuliwa na Ukimwi pamoja na magonjwa nyemelezi," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali ilimua kufanya utafiti kwa lengo la kujua hali ya sasa ya VVU na Ukimwi ilivyo nchini na matokeo yanaonyesha Tanzania imepata mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya Ukimwi.

Kutokana na matokeo ya utafiti huo, Waziri Mkuu alitoa maagizo kwa vijana nchini kuanza kujitambua na kutathimini maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU.

" Ninawaomba wadau wote kuweka kipaumbile katika kundi hili la vijana ili kulinusuru na athari za Ukimwi " alisema.

Waziri Mkuu pia aliwataka watu wanaishi na VVU kuendelea kutumia dawa za ARV kwa usahihi bila kuacha na kuimarisha afya zao kwa kuwa taifa linawategemea wakati serikali ikiendelea kuhakikisha huduma za ARV zinaendelea kupatikana.

Aliagiza mikoa na wilaya zote nchini kutekeleza maelekezo ya kufanya maadhimisho ya siku ya ukimwi Duniani na kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Pia aliwaomba kuwaomba viongozi wa dini, kisiasa na kimila kutumia majukwaa walio nayo kuendelea kusema na kukemea taarifa za ubaguzi dhidi ya Waviu na kuhimiza upendo na huruma kwao.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, kwa kushirikiana na waziri mwenzake anayeshughulikia, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu pamoja na Waziri wa Afya alisema watajipanga kuhakikisha wanawalinda vijana dhidi ya janga la Ukimwi.

Naye Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema ili kukabilina na kasi ya maambukizi ya VVU, wizara imezindua mpango wa kuunganisha VVU, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini kwa kuwa hushabiana kwa kiasi kikubwa katika njia za maambuki ya magonjwa hayo.

# Othman ataka iwe ajenda utendaji kazi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka taasisi za serikali, wizara, mashirika, sekta binafsi, asasi za kiraia na vyombo vya habari kuweka kipaumbele suala la Ukimwi katika shughuli zao za kila siku.

Amesema masuala ya Ukimwi yanapaswa kuzingatiwa ipasavyo katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za taasisi hizo ikiwa ni jithada za pamoja za kupambana na tatizo hilo nchini.

Othman aliyasema hayo huko Nungwi, mkoa wa Kaskazini Unguja, alipohutubia katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kitaifa kwa Zanzibar yaliadhimishwa katika viwanja vya Skuli ya Nungwi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kwa taasisi hizo kuzifikia vyema jamii zinazozihudumia na kusaidia kutoa elimu na miongozo ya ndani itakayowasaidia wafanyakazi kujikinga na maambukizi ya Ukimwi wao na familia zao.

Zanzibar, alisema ni sehemu ya duania na endapo suala la Ukimwi halitaendelea kushughulikiwa ipsavyo, hali iliyopo sasa Zanzibar ya kiwango cha mambukizi ya chini ya asilimia moja, inaweza kubadilika na kusababisha madhara makubwa.

Othman alisema katika kupambana na janga hilo, taasisi zote na mwananchi mmoja mmoja, zina wajibu wa kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya Ukimwi kwa vile sera, sheria na mikakati inazitaka taaisisi zote nchini kuchukua hatua katika kupambana na tatizo hilo kwa nafasi zao.

Alisema ili kushinda vita dhidi ya Ukimwi ni lazima kuwapo ushiriki sahihi wa jamii yote na kwamba ili hayo yawezekane, mapambano dhidi ya Ukimwi yaingizwe katika mipango ya kila mwaka ya utekelezaji ya taasisi hizo.

Othman pia aliziagiza Tume ya Ukiwmi, Kitengo Shirikishi cha Wizara ya Afya, washirika wa maendeeo na wadau wengine kuzifanyia kazi takwimu za utafiti wa maradhi hayo ili zisaidie katika jitihada za kuongeza ufanisi kwenye mapambano ya kuzuia maambukizi mapya.

Kuhusu hali ya mambukizo ya VVU Zanizbar, Othman alisema watu 10,580 sawa na asilimia nne ya Wazanzibari, wanaishi na virusi vya maradhi hayo Unguja na Pemba kiwango ambacho ikilinganishwa na idadi ya watu ni kikubwa, hivyo kunahitajika jitihada za kila mmoja kuzuia mambukizi mapya.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za utafiti zilizoko kisiwani Unguja zinaonyesha ndiko kwenye maambukizi makubwa zaidi kulinganisha na Pemba.

Takwimu zinaonyesha kuwa Pemba wanaoishi na virusi ni asilimia 0.3 wakati Unguja ni asilimia 0.5 huku mkoa wa kusini Unguja ukiongoza kwa asilimia 0.8 ukifuatiwa na Kasazini Unguja wenye asilimia 0.7 ya maambukizi.

Pia alisema utafiti wa mwaka wa 2023 unaonyesha kuwa wanawake wanaofanya biashara ya ukahaba Zanzibar, kiwango cha maambukizi ni asilimia 21.1 huku wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja wakiwa na maambukizi kwa asilimia 11.2 na waraibu wa dawa za kulevya wakiwa na kiwango cha asilimia 9.4.

# Mhandisi Luhemeja aanika mafanikio ujenzi kiwanda cha sukari Mkulazi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja, amepongeza kazi kubwa iliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya kujenga kiwanda cha sukari Mkulazi, mkoani Morogoro.

Mhandisi Luhemeja alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi za NSSF zilizoko katika Jengo la Benjamini William Mkapa, Dar es Salaam na kuzungumza na menejimenti ya mfuko huo.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho ambacho kimeanza uzalishaji ni hatua kubwa kwa taifa kwa sababu kitaongeza upatikanaji wa sukari, kitazalisha ajira kwa Watanzania na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Ujenzi wa kiwanda hiki ni hatua kubwa sana kwa nchi yetu kwa sababu kitaleta tija kwa NSSF, taifa na jamii kwa ujumla," alisema.

Mhandisi Luhemeja alisema faida nyingine ya kiwanda hicho ni kuwa kimezalisha ajira za moja kwa moja 11,000 jambo ambalo mfuko pia umeongeza kiwango cha ajira kwa Watanzania na kwamba katika awamu ya kwanza kitazalisha tani za sukari 50,000 lakini lengo ni kuzalisha tani 75,000.

"Haya ambayo yamefanywa na NSSF katika kiwanda hiki ni mapinduzi makubwa sana na ukiangalia sera ya mfuko inataka tuwekeze kwenye maeneo yenye tija kama haya," alisema.


Akizungumzia uwekezaji wa majengo, alisema NSSF pia inafanya vizuri kwa kujenga majengo mazuri na yenye viwango, huku akionyesha kuvutiwa na uwekezaji wa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano iliyoko jijini Mwanza.

Katika hatua nyingine, Luhemeja aliipongeza NSSF kwa kuendelea kufanya vizuri katika kutekeleza majukumu yake ya msingi huku akiiomba Menejimenti kuendelea kuongeza kasi ya kuandikisha wanachama wapya ili kuongeza idadi ya wanachama wachangiaji.

Mhandisi Luhemeja aliiomba NSSF kushirikiana na taasisi zingine kama Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ili kuunganisha nguvu ya pamoja kwa lengo la kusajili waajiri na wafanyakazi wengi zaidi.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alimshukuru Mhandisi Luhemeja kwa ziara hiyo na kuahidi kuwa maagizo na maelekezo yake yatafanyiwa kazi hasa katika kuongeza idadi ya wanachama wachangiaji.

Alisema mfuko unaendelea kuboresha huduma zake kwa kutumia mifumo mbalimbali ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kuwarahisishia wanachama na wadau kupata huduma kwa urahisi popote walipo bila ya kulazimika kufika katika ofisi za NSSF.



Mufti wa Tanzania Shekhe Dk. Abubakar Zubeir Bin Ally (kulia), akitoa ufafanuzi wa jambo kwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikati na Uenezi, Paul Makonda (wa pili kulia), alipomtembelea ofisini kwake katika Msikiti wa Mfalme wa Morocco Muhammad VI, Kinondoni Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gwajima akiri ukatili janga kubwa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii Wanawake Watoto na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema kuwa ukatili wa kijinsia na watoto nchini ni janga kubwa linalosababisha serikali kushindwa kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo.

Amesema hali hiyo inatokana na fedha nyingi kutumika katika utoaji wa elimu na kusaidia wanawake na watoto waliofanyiwa ukatili.

Dk. Alisema hayo juzi mkoani hapa wakati akifunga tamasha la kitaifa la kutangaza fursa za kiuchumi na kupinga ukatili nchini (Tanzania Development Festivals) lilofanyika mjini Geita.

Alisema Watanzania hawana budi kuungana kupaza sauti zao kupinga matukio hayo ili kuokoa rasilimali kubwa zinazotumiwa na taifa.

Dk. Gwajima alisema wizara kwa kushirikia na taasisi ya mabalozi wa kupinga ukatili wa kijinsia na watoto nchini (FAGDI) imeanzisha tamasha hilo la kitaifa lenye kauli mbiu zijue fursa imarisha uchumi kataa ukatili kazi eendele litakalo zunguka nchi nzima likiwa na lengo la kutanga fursa za kiuchumi na kupinga ukatili.

"Watoto nao wamekuwa wakifanyiwa ukatili ikiwamo kupigwa na kujeruhiwa na wazazi wao, hivyo bila kushirikiana kwa pamoja hatuwezi kufanikiwa katika mapambano ya kukomesha matukio ya ukatili. Dawa pekee ni kukataa kufumbia macho matukio ya ukatili," alisema.

Dk. Gwajima alisema kwa mujibu wa ripoti ya shirika la kutetea wanawake duniani, matukio hayo huathiri hali ya uchumi duniani kwa asilimia mbili kutokana na kusaidia waathirika wa matukio hayo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema ukatili wa kijinsia umeongezeka kwa kasi na wanawake nao kwa sasa wanawafanyia ukatili waume zao.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Mohamed Gombati, alisema katika kipindi cha kuanzia robo ya mwaka 2023, matukio ya ukatili yameripotiwa 343 kati hao watoto wa kike ni 67 na wa kiume 16 na wanawake 187 wamefanyiwa ukatili wa aina mabalimbali ikiwamo kupingwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa FAGDI na Mwenyekiti wa mabalozi wa kupinga ukatili wa kijinsia na watoto nchini, Simon Mwapagata, alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na mabalozi hao kwa pamoja watahakikisha wanatembea nchi nzima lengo ni kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia nchini.

Awali, Mratibu wa Tamasha hilo kitaifa, Dk. Neema Obwana, kutoka Wizara ya Maendeleo Jamii, alisema tamasha hilo kitaifa lilizindulwa Aprili 24, mwaka huu, jijini Dodoma na mkoani Geita lilianza Novemba 25.

# Balozi ataja vikwazo kukuza usawa kijinsia

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI wa Uswisi nchini Tanzania, Didier Chassot, amesema mila na desturi na hali ngumu ya kiuchumi bado ni kikwazo katika kukuza usawa wa kijinsia, hivyo kuongeza changamoto kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu kutimiza wajibu wao.

Balozi Chassot aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Binadamu, iliyoandaliwa na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (CWHRD).

Katika miongo kadhaa iliyopita, alisema mifumo ya kisheria ya kimataifa na kitaifa imeimarishwa ili kukuza usawa wa kijinsia utekelezaji bado haujafanikiwa.

Alisema kazi ya watetezi wa haki za binadamu ina umuhimu mkubwa inasaidia kutathmini matumizi bora ya haki za binadamu ili kuzikuza, kuzisukuma na kuzilinda inapohitajika.

Balozi alitoa wito kwa mataifa yote kuheshimu kundi hilo na kuwapa ulinzi, hasa wale wanaolengwa kwa misingi ya jinsia au utambulisho wao na kukabiliwa na shinikizo la kuongezeka.

"Wanawake watetezi wa haki za binadamu katika maeneo mengi wanakabiliwa na vitisho maalum vya kijinsia kama vile mashambulizi ya kijinsia, ubakaji au aina nyingine za unyanyasaji wa kijinsia kwa kupinga kanuni za kitamaduni za kijamii. Wanawake, watetezi wa haki za binadamu au binadamu pia wako katika hatari ya kunyanyapaliwa katika jamii zao," alisema.

Alisema Tanzania inastahili pongezi kwa hatua iliyofikiwa katika kupunguza pengo la kijinsia, kwani ripoti ya Jukwaa la Uchumi la Dunia inaonyesha kuwa mwaka huu, iliboresha nafasi yake katika ripoti ya Global Gender Gap, ikitoka nafasi ya 60 mwaka jana kati ya 146 kushika nafasi ya 45.

Balozi huyo alisema Uswisi imejitolea kuchangia katika kuimarisha utawala unaojumuisha jinsia na taasisi za umma, kuongeza ushiriki wa wanawake katika maamuzi na kutoa maoni ili kuboresha maisha ya vijana wa kike nchini Tanzania.

Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU) wa Siasa, Vyombo vya Habari, Sarah Torp, alisema licha ya juhudi za kutekeleza tamko la Marrakesh, watetezi wa haki za binadamu wanaendelea kukabiliwa na changamoto nyingi, hivyo zinahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa washirika wa kitaifa na kimataifa, asasi za kiraia na jamii za mitaa.

Alisema juhudi hiyo zitasaidia kuendeleza kazi zao na kupambana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mwaka 2015, alisema EU ilizindua utaratibu wa ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu ili kusaidia kundi hilo hadi sasa mpango huo umetoa msaada kwa zaidi ya 60,000 wa haki za binadamu na wanafamilia zao wakiwemo waandishi wa habari.

Mkurugenzi wa UN Women nchini, Hodan Haddou, alitoa wito kwa wadau wa haki za binadamu kuthibitisha uungaji mkono kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu, ili kutambua juhudi zao na kuweka njia kuelekea ulimwengu wenye usawa zaidi, jumuishi na haki kwa wote.

Mkurugenzi wa Idara ya Haki za Binadamu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Anne Malipula, alisema katika jitihada za kuleta usawa wa kijinsia mwaka 2004, serikali ilianzisha dawati maalum la kushughulikia elimu kwa umma na haki za wanawake nchini.



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (kulia), akikata utepe kuzindua kitabu kiitwacho "Utawala Bora" kilichoandikwa na Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania, Barnabas Samatta (kushoto), jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mkurugenzi wa Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Felista Mauya. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jaji Samatta asisitiza haki, utawala bora

**Na Sabato Kasika**

JAJI Mkuu Mstaafu wa Tanzania, Barnabas Samatta, amezindua kitabu chake kiitwacho 'Utawala Bora', huku akitaja sababu za kuandika kuwa ni kutaka kuona haki inatendeka katika kila nyanja ili kuimarisha utawala bora. Uzinduzi wa kitabu hicho ulifanyika jijini Dar es Salaam juzi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa mambo ya sheria, akiwamo Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma.

"Napenda kuelezea kile ambacho kimenisukuma kuandika kitabu hiki kwamba utawala bora hauwezi kuwa tu falsafa. Kila kiongozi ndani awe wa serikali lazima awajibike kikamilifu kusimamia utawala bora," alisema. Jaji Samata alisema katika kufanikisha utawala bora, utendaji haki ni muhimu Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na vituo vya kupigia kura kuwapo haki kwa mabunge na taasisi za kutunga sheria. "Vilevile ni muhimu kuwapo haki katika ofisi za serikali kuu na taasisi zake lakini pia kuwapo haki ndani ofisi za serikali za mitaa," alisema. Jaji Mkuu huyo mstaafu alisema anatamani pia kuona haki inatendeka katika vyombo vya utoaji haki, pamoja na haki za wananchi kulindwa dhidi ya uonevu, uovu na rushwa.

"Lakini pia haki ya wananchi kuheshimiwa na uongozi wa nchi yao, haki yao ya kushirikishwa katika uamuzi unaohusu nchi," alisema huku akisema anatamani kuona yaliyomo katika kitabu chake yanaendelezwa ili yatoe mchango kwa maendeleo ya nchi.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Juma aliwataka wadau kununua kitabu hicho ili kujiongezea ujuzi katika utendaji kazi wao.

"Nimekipitia kitabu hiki kina mambo mengi ya kujifunza. Umetumia uzoefu wa kukiandika, hivyo niseme tu kuwa ni vyema kila mmoja akapata nakala yake," alisema Prof. Juma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema kitabu hicho kimekuja wakati sahihi na kwamba ni muhimu Watanzania wakipate. "Utawala bora una nafasi kubwa katika maendeleo ya nchi. Ni sehemu ya haki za binadamu, utawala bora hakuna unyanyasaji, kunakuwa na sheria nzuri ambazo si kandamizi," alisema.

# Maboresho makubwa mfumo sera ya kodi

**Na Peter Haule,** MBEYA

Serikali imesema itakuwa inafanya marekebisho ya kodi kila baada ya miaka mitatu ili kuwa na sera ya kodi inayotabirika na kuwafanya wawekezaji kuweka mipango yenye ufanisi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, alisema hayo jana wakati wa Kongamano la Ukusanyaji Maoni ya Kodi Kikanda jijini hapa ikiwa ni mwendelezo wa makongamano kama hayo yanayofanyika katika kanda mbalimbali kwa lengo la kuboresha Sera ya Kodi kwa mwaka 2024/25.

Alisema utaratibu wa sasa ni kufanya marekebisho ya kodi kila baada ya miaka mitatu, hivyo marekebisho yaliyofanywa mwaka huu hayafanyiki tena hadi miaka mitatu ili kuwa na Sera za Kodi inayotabirika.

"Awali kulikuwa na utaratibu uliosababisha wananchi kusema bajeti ni ya pombe, sigara na soda. Maana ya kauli hizo ni kuwa kila mwaka serikali ilikuwa inabadilisha viwango vya kodi vilivyokuwa vinatozwa kwenye bidhaa hizo jambo ambalo kwa sasa halitakuwa linafanyika kila mwaka", alisema.

Kuhusu maboresho ya kodi yaliyofanyika, Mwandumbya alisema serikali imeongeza bidhaa za mtaji (capital goods) zinazozalishwa nchini katika wigo wa ahirisho la kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kuanzia Julai Mosi, 2023 na kuondoa katika wigo huo bidhaa za mtaji zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kuanzia Julai Mosi, 2026.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

## TANGAZO KWA UMMA

**KUSAINI MIKATABA YA MALIPO YA FEDHA ZA KUSAIDIA KUPATA ARDHI MBADALA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Serikali, kupitia tamko la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI la tarehe 15/11/2023, imeamua kuwalipa waathirika wote wanaohamishwa malipo sawa kwa ajili ya kuwasaidia kupata ardhi mbadala. Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo sawa kwa ajili ya kupata ardhi mbadala kwa waathirika wote ambao wameafiki malipo yao katika zoezi la mwezi Oktoba 2023. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata na Mtaa kwa ratiba ifuatayo:

| KATA | MITAA INAYOHUSIKA | TAREHE |
|---|---|---|
| Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 6 hadi 7/12/2023 |
| | Misheni Kota | 8 hadi 9/12/2023 |
| | Ilala Kota | |
| Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| Upanga Magharibi | Charambe | 10 hadi 11/12/2023 |
| Jangwani | Mtambani A | |
| | Mtambani B | |
| Magomeni | Suna | 12 hadi 14/12/2023 |
| Mzimuni | Idrisa | |
| | Mtambani | |
| | Mwinyi Mkuu | |
| Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 15 hadi 16/12/2023 |
| Hananasifu | Mkunguni A | |
| | Mkunguni B | |
| | Hananasifu | |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Twiga Stars nendeni Togo kumaliza kazi, msibweteke

**TIMU** ya Soka ya Taifa ya Wanawake maarufu kwa jina la Twiga Stars, iko katika kinyang'anyiro cha kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), ambazo zitafanyika Morocco.

Twiga Stars imewahi kucheza fainali hizo mara moja tu, ilikuwa ni mwaka 2010, ambapo mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) yalifanyika katika jiji la Johanesburg, Afrika Kusini.

Kikosi hicho wakati huo kilikuwa chini ya Kocha Mkuu Mzalendo, Boniface Mkwasa 'Master' na nahodha wake akiwa ni Sophia Mwasikili, ambaye sasa ni Kocha Msaidizi wa Simba Queens, iliyocheza hatua ya nusu fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, iliyofanyika mwaka jana nchini Morocco.

Wawakilishi hao ambao sasa wako chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime 'Mchawi Mweusi', wanapambana kusaka tiketi hiyo ili kuwapa Watanzania furaha ya kushiriki fainali hizo ambazo wamekuwa wakizisubiri kwa zaidi ya miaka 10, na wanaamini mwaka huu ndoto zinaweza kutimia.

Twiga Stars imeanza vyema raundi ya tatu na ya mwisho kwa kupata ushindi wa mabao 3-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na tayari imeshafajiri kuwafuata wenyeji wao Togo kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaofanyika keshokutwa.

Mechi hiyo iliyokuwa na ushindani ikichezeshwa na waamuzi kutoka Malawi, ilikuwa ngumu kuanzia mwanzo, lakini wenyeji wakionekana kutoelewana na uhai wao ulianza kuonekana kipindi cha pili kutokana na mabadiliko yaliyofanywa, mchezo huo umekwisha na kila upande unawafahamu wapinzani wao.

Kikubwa na jambo la msingi ni benchi la ufundi la Twiga Stars pamoja na Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi ya kwanza ili kulinda ushindi na hatimaye kufuzu kucheza WAFCON 2024.

Haipaswi kabisa kubweteka na ushindi huo kwa sababu Togo nao wataingia uwanjani wakiamini wanaweza kukifanya kile ambacho Watanzania wamekifanya Dar es Salaam na hivyo kujiweka kwenye hatari, licha ya kutangulia kupata mtaji mzuri wa mabao.

Twiga Stars inatakiwa kuweka mawazo ya kuhitaji kushinda katika mechi hiyo ya ugenini kama walivyofanya nyumbani, inatakiwa kucheza kwa kupambana na kujituma wakati wote, lakini pia ikiwaheshimu wapinzani wao kutokana na hatua ambayo wamefika.

Kama walivyotumia nguvu, umakini na kujituma katika mechi ya kwanza, wachezaji wa Twiga Stars wanatakiwa kuziongeza ili kumalizia dakika nyingine 90 zilizobakia ambazo kwa hakika zitabadilisha historia na maisha yao kwa sababu ya kupokea motisha kutoka kwa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Awali ilionekana ngumu kwa timu kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kuziondoa katika mashindano hayo ya kimataifa ya CAF, vigogo kutoka Afrika Magharibi, lakini sasa dunia imebadilika na kinachotakiwa ni wachezaji kuongeza nguvu na umakini na hatimaye kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Tunawakumbusha wachezaji kufahamu kufanya vyema katika mechi hiyo ya marudiano na kufuzu WAFCON, kutawapeleka sokoni kwa sababu mawakala na makocha wa timu mbalimbali kutoka Ulaya wanatarajiwa kufika kwenye fainali hizo kusaka nyota wa kuwasajili ili kwenda kuboresha vikosi vyao.


Endapo Twiga Stars itafuzu kucheza fainali hizo, hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa timu za Tanzania kucheza michuano hiyo pamoja baada ya kaka zao, Taifa Stars kutangulia kukata tiketi ya kushiriki AFCON hapo mwakani, na heshima hiyo ataipata pia Rais Samia ambaye ameshiriki katika maandalizi ya vikosi hivyo.

Nipashe inaitakia kila la kheri Twiga Stars katika mbio hizo za kuisaka tiketi ya kushiriki WAFCON 2024.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Simba SC, Yanga ushindi unawezekana mechi CAF

**HAZIKUPATA** ushindi katika mechi zao za kwanza kwenye hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika zilizochezwa wiki iliyopita.

Yanga ilikutana na kipigo cha mabao 3-0 ugenini nchini, Algeria dhidi ya CR Belouizdad na kesho yake, Simba ilishindwa kuutumia vizuri uwanja wa nyumbani, Benjamin Mkapa dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast na kulazimishwa sare ya bao 1-1.

Matokeo ya mechi hizo ni kama vile yameanza kuwatisha baadhi ya mashabiki wenye roho ndogo huenda timu za Tanzania, Simba na Yanga zisitoboe kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Wanalinganisha na mechi za raundi ya pili zinazochezwa leo, ni ngumu kwa timu zote mbili.

Pamoja Yanga ipo nyumbani, lakini inacheza na mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Al Ahly kutoka Misri huku Simba ikiwa ugenini ikionyeshana kazi na timu machachari ya Botswana, Jwaneng Galaxy ambayo 2021 iliisukumiza nje ya michuano hiyo kwa faida ya bao la ugenini.

Simba iliifunga Jwaneng Galaxy mabao 2-0 huko Botswana, lakini katika hali ambayo haikutarajiwa ilikutana na kipigo cha magoli 3-1 katika mechi ya marudiano nyumbani na kuifanya kushindwa kutinga hatua ya makundi.

Leo timu hizi zinakutana tena zikiwa kwenye hali mbili tofauti, Jwaneng Galaxy ikionekana kujiimarisha zaidi na inajionyesha dhahiri kwa kuifunga Wydad Casablanca bao 1-0 nyumbani kwao Morocco, huku Simba ikionekana kama vile imekuwa ya kungaunga.

Pamoja na yote haya, lakini ushindi kwa timu zote za Tanzania inawezekana.

Yanga ambayo kwa misimu miwili imekuwa na kiwango bora, na wachezaji wanaopambana na kujituma, wakiongozwa na maelfu ya mashabiki watakaojitokeza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wanaweza kabisa kupata ushindi katika mechi ya leo usiku.

Nguvu ya Yanga ipo kwa viungo wao Pacome Zouzoua, Maxi Nzengeli na Stephane Aziz Ki ambao walidhihirisha hilo hata mechi iliyopita huko Algeria, kwa sababu ni wana uwezo mkubwa wa kukaa na mpira mguu, kutengeneza nafasi na hata kufunga.

Yanga pia ina viungo wakabaji asilia ambao wana uwezo mkubwa wa kuwafichia mabeki makosa yao.

Iwapo ufundi utaongezwa kidogo tu, hapana shaka Yanga inaweza kupata ushindi kwa kuwafunga Waarabu hao wa Misri kwa mara ya pili kama ilivyofanya Machi Mosi, mwaka 2014 kwenye uwanja huo huo, iliposhinda bao 1-0 lililofungwa na Nadir Haroub 'Cannavaro', dakika nane kabla ya mechi kumalizika ikiwa ni mechi ya raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa upande wa Simba inaonekana kuna vitu fulani tu wachezaji wanakosa. Labda walikuwa hawafanyi kabisa au walikuwa wakifanya mazoezi madogo ya stamina na pumzi, ndiyo maana wanaonekana wanapata tabu sana kipindi cha pili hasa kuanzia dakika ya 70.

Simba ina wachezaji wazoefu na michuano ya kimataifa wenye uwezo wa kucheza uwanja wowote ule Afrika bila hofu na kupata ushindi.

Kama walishinda Oktoba 17, mwaka 2021 ugenini kwa mabao 2-0 yaliyofungwa na Thadeo Lwanga na John Bocco, sidhani kama inaweza kushindwa kufanya hivyo leo huko Francistown.

Bahati pekee iliyokuwa nayo Simba ni kumnasa kocha mpya, Abdelhak Benchikha, ambaye atakuwa akiangalia pia viwango vya wachezaji wake kwa mara ya kwanza baada ya kutua klabuni hapo.

Mara nyingi wachezaji hujituma zaidi anapokuja kocha mwingine ili kumshawishi, na hili ndilo mashabiki wengi wa Simba wanalotarajia, hali ambayo itawafanya kupambana na kuipatia timu ushindi.

Kila la heri timu za Tanzania katika mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

HABARI KITAIFA




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akizungumza katika uzinduzi wa maadhimisho ya kitaifa ya Tutembee Pamoja na Kupambana na Ukatili wa Kijinsia Kimkoa katika Uwanja wa Jitegemee, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi kwa udhamini wa FEMINA. Katikati ni Balozi wa Ireland nchini, Mary O'Neil na (kulia) ni Katibu Tawala wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Dira maendeleo 2050 kulenga uchumi jumuishi

**Na Restuta James**

KATIBU Mtendaji wa Tume ya Mipango, Lawrence Mafuru, amesema Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 itajikita kujenga uchumi jumuishi kwa kuweka mipango madhubuti ya kuchochea sekta za kilimo, uvuvi, mifugo na uzalishaji viwandani zinazoajiri Watanzania wengi.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kufungua mkutano wa kwanza wa kitaifa wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na kuzindua timu kuu ya kitaalamu ya dira, kamati ya usimamizi wa dira pamoja na nyenzo za kidijitali zitakazotumika kukusanya maoni ya wadau.

Mafuru alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, kuhusu Mkutano Mkuu wa kwanza wa dira 2050, utakaofanyika Desemba 9, mwaka huu.

Alisema katika tathmini ya dira ya maendeleo 2025, serikali imetambua umuhimu wa ukuaji wa uchumi ambao ni jumuishi ili malengo ya dira yaweze kugusa uhalisia wa maisha ya wananchi wengi zaidi.

"Tunaposema tuwe na uchumi jumuishi ni kwamba kweli kuna sekta za uchumi zinazokua lakini unapoangalia wanaonufaika na ukuaji wake ni wachache. Kwa mfano, mojawapo ya sekta zinazochangia ukuaji wa uchumi wetu kwa sasa ni ujenzi wa miundombinu lakini ni Watanzania wachache wanaoshiriki," alisema Mafuru.

"Ili kuwa na ukuaji wa uchumi ambao ni jumuishi, serikali inaelekeza rasilimali kwenye sekta ambazo zitaleta ujumuishi... tukiweka ukuaji zaidi kwenye kilimo, watu wengi zaidi watanufaika. Tunarekebisha hiyo kasoro ambayo imejitokeza inayoonesha uchumi unakua lakini wachache wanaonufaika ili ukuaji uguse watu wengi zaidi," alifafanua.

Mafuru alisema mikakati ni kuziimarisha sekta hizo na kuweka mazingira ya ujenzi wa viwanda vingi ili ajira zaidi zizalishwe ili watu wapate vipato.

Waziri Mkumbo alisema taarifa ya kitafiti ya tathmini ya dira ya maendeleo 2025, imeainisha changamoto na mafanikio huku ikionyesha kuwa pato la Mtanzania limekua kutoka Sh. 322,597 mwaka 2000 hadi Sh. 2,880,000.

"Tanzania imefikia asilimia 124 ya kujitosheleza kwa chakula ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 140 ifikapo mwaka 2025. Hatua hii imewezesha Tanzania kukabiliana na njaa kwa mikoa na wilaya zote nchini.

"Mtandao wa barabara za lami na zege katika mikoa umeongezeka kutoka kilometa 4,179 mwaka 2000 hadi kilometa 11,966.38 mwaka 2023...tumefanikiwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 760 kwa vizazi hai 100,000 mwaka 2000 hadi vifo 104 mwaka jana," alisema.

Kuhusu mkutano wa kwanza wa dira 2050, Prof. Mkumbo alisema utahudhuriwa na zaidi ya wadau 900 wakiwamo viongozi wakuu wa serikali ya Muungano na ya Zanzibar, mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wa mikoa, viongozi wa vyama vya siasa na dini, makundi maalumu kama wafugaji, wakulima, wazee, wenye ulemavu na wavuvi.

"Kwa kuwa mkutano huu unafanyika siku ya Uhuru, Mheshimiwa Rais anatarajiwa kutumia siku hii kutoa ujumbe maalum katika kuadhimisha miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara," alisema.

## Wananchi wengi Mikoani kufikiwa huduma kifedha

**Na Faustine Feliciane**

WANANCHI wengi wanatarajiwa kufikiwa na huduma za kifedha karibu zaidi baada ya makubaliano ya ushirikiano baina ya benki ya DCB na kampuni ya simu za mkononi ya Tigo yaliyotiwa saini juzi jijini Dar es Salaam.

Katika ushirikiano huo mpya, wateja wa benki hiyo wanaweza kufanya miamala yao kupitia huduma za Tigopesa inayotolewa na kampuni ya Tigo.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa huduma hiyo, Mkurugenzi wa Sheria wa DCB, Regina Mduma, kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, alisema kuwa matawi 10,000 yatapatikana kupitia mawakala wa Tigopesa ambao watakuwa wakitoa huduma za benki ya DCB kwa wateja nchini kote.

"Lengo letu ni kuwarahisishia huduma wateja wetu. Pale ambapo hakuna tawi la DCB, mteja bado anaweza kupata huduma zetu kupitia wakala wa Tigopesa," alisema Mduma.

Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha, alisema ushirikiano huo una lenga kufikisha huduma za kifedha karibu kabisa na wananchi.

Alisema kampuni za simu zina mchango mkubwa katika kusaidia kufikisha huduma hizo za kifedha sehemu wananchi walipo hapa nchi na kusaidia serikali.

"Tigopesa inahudumia zaidi ya watu milioni 16. Ushirikiano huu utafanya kuwapo na mawakala 10,000 waliochaguliwa ambao watatoa huduma za kifedha za benki ya DCB kupitia huduma hii mpya tuliyozindua hii leo (juzi)", alisema Pesha.

Alisema kampuni hizo bado zitaendelea kushirikiana kuhakikisha wanawarahisishia mambo wateja wao popote walipo na bado zipo huduma nyingine za ushirikiano zinakuja kwa siku za usoni.

# Serikali yaahidi mazingira wezeshi biashara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imeahidi kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wazalishaji, wafanyabiashara na wenye viwanda ili kukuza uchumi wa nchi.

Hatua hiyo inalenga kutimiza dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara nchini kwa kuboresha mifumo ya uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa mipango, mikakati na program mbalimbali za kisekta ili kufikia malengo ya kiuchumi na kijamii ya maendeleo endelevu na ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashi Abdallah, kwenye Makao Makuu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dar es Salaam na kwenye Maadhimisho ya Siku ya Viwango Duniani alisema sekta za viwanda na biashara ni moja ya mihimili mikubwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuchangia katika pato la Taifa, kutokana na bidhaa za viwandani zinazozalishwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi, pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania.

Kutokana na umuhimu huo, Dk. Abdallah aliwataka wadau wote kila mmoja katika nafasi yake kuendelea kushirikiana na TBS, kwa kutoa msaada na uzoefu katika taaluma yake ili kuchangia ipasavyo katika utengenezwaji wa viwango nchini, kwani TBS ni moja ya mashirika ya umma bora yanayoheshimika nchini, ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na Afrika nzima.

Dk. Abdallah alisema TBS imekabidhiwa mamlaka ya kutengeneza na kusimamia utekelezaji wa viwango nchini, kwani viwango ni muhimu katika kuendeleza sekta ya viwanda na biashara nchini.

Alitoa rai kwa wadau na wananchi kwa ujumla kushiriki na kutoa maoni katika mchakato wa uandaaji na utengenezaji viwango ili vikidhi mahitaji ya jamii yetu.

Akizungumzia maadhimisho ya Siku ya Viwango Duniani, Dk. Abdallah alisema ni muhimu kwani ni njia mojawapo ya kuenzi juhudi shirikishi za maelfu ya wataalamu duniani ambao hutengeneza mikataba ya hiari na lazima ya kiufundi ambayo huchapishwa kama viwango vya kitaifa na kimataifa ili kulinda afya za walaji na mazingira.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema wanatambua juhudi za wadau na mchango mkubwa wa kujitolea katika kuandaa viwango na hatimaye kuhakikisha afya za watanzania na mazingira vinalindwa na pia kukuza biashara.

Alisema tangu kuanzishwa kwake hadi leo TBS kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanikiwa kuandaa viwango zaidi ya 4,000.

"Viwango hivi ni pamoja na vile vinavyobainisha matakwa ya usalama, matakwa ya utengenezaji, matakwa ya matumizi pamoja na kanuni za upimaji vyote vikiwa na lengo la kuboresha bidhaa na huduma," alisema Dk. Ngenya.

Alisema kwa takwimu wataalamu hao kwa mwaka huandaa, kupitia na kurejea viwango zaidi ya 500.

"Kazi hii hufanywa kwa kujitolea muda wao na kushirikiana na maofisa viwango na wadau wengine hakika shirika linatambua mchango wao mkubwa," alisema Dkt. Ngenya.

Alisema kwa kuwa wanaelekea katika Maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika (ARSO) Machi, mwakani ARSO imejikita kuhuwianisha viwango barani Afrika yenye lengo la kupunguza vikwazo vya kiufundi ili kuimarisha biashara kati ya nchi za Afrika.

# Sweden yaisaidia Tanzania bil. 210/- kuimarisha elimu

**Na Waandishi Wetu**

TANZANIA na Sweden, kupitia Taasisi ya Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE) na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Kimaendeleo la Sweden (SIDA), zimetia saini mkataba wa msaada wenye thamani ya dola za Marekani milioni 84 sawa na Sh. bilioni 210, kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Kada ya Ualimu nchini.

Mkataba huo ulitiwa saini juzi jijini Dar es Salaam kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dk. Natu El-maamry Mwamba, na Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Marcias.

Dk. Mwamba alisema katika fedha hizo za msaada, dola za Marekani milioni 29.3 zitatumika kuboresha mchakato wa ukusanyaji takwimu za elimu; kuboresha elimu ya walimu, ajira, maendeleo endelevu ya kitaaluma, motisha na uwajibikaji.

Pia alisema dola za Marekani milioni 54.8 zitatumika kufadhili shughuli zinazotegemea matokeo, ili kuinua nguvu kazi ya walimu, usawa wa kijinsia, ushirikishwaji, na mazingira ya ufundishaji na kujifunza shuleni kwa lengo la kuchochea mabadiliko ya kimageuzi kwa kada ya ualimu ambayo itaongeza ufanisi katika mfumo wa elimu ya msingi.

Dk. Mwamba alisema mkataba huo utaongeza misaada kutoka GPE nchini Tanzania kufikia dola za Marekani milioni 309, sawa na takriban Sh. bilioni 773 na kwamba fedha hizo zimekuwa nguvu inayoendesha mabadiliko chanya katika mfumo wa elimu, ukigusa maisha ya wengi.

"Tunashukuru kwa michango ya kipindi kilichopita. Tanzania ilipata misaada kupitia fedha za GPE jumla ya dola za Marekani milioni 225 sawa na takriban Sh. bilioni 562 zilizotumika kugharamia utekelezaji wa programu ya kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa awamu ya kwanza kuanzia mwaka 2013 hadi 2018 na awamu ya pili kuanzia 2019 hadi 2024," Alisema Dk. Mwamba

Dk. Mwamba aliihakikishia Sweden kuwa dhamira ya serikali ya Tanzania ni kuendelea kufanya kazi kwa karibu na nchi hiyo, GPE na washirika wote wa maendeleo ili kuimarisha ushirikiano wa kimaendeleo.

Balozi Marcias alisema tangu Tanzania ijiunge na GPE mwaka 2013, sekta ya elimu imeboreshwa ikiwamo kupungua kwa msongamano wa wanafunzi wa shule za msingi madarasani kutoka wastani wa wanafunzi 113 hadi 50.

Alisema serikali yake itaendelea kutimiza wajibu wa kuwa wakala wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuiwezesha Tanzania kutimiza wajibu wake wa kuboresha mifumo ya elimu nchini ili kuyanufaisha makundi ya walimu kwa kuwajengea ujuzi, maarifa, kuwapa motisha, ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya elimu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa GPE, Laura Fringent, aliipongeza Tanzania kwa hatua kubwa iliyopiga katika maendeleo ya sekta ya elimu na kuahidi kuwa Taasisi yake, itaendelea kutoa mchango wa kuboresha mazingira ya walimu nchini ili kuboresha zaidi elimu kwa faida ya maendeleo ya taifa.

Awali, akitoa maelezo ya mpango huo wa kuboresha elimu kupitia walimu unaofadhiliwa na GPE, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (-TAMISEMI), Prof. James Mdoe, alisema msaada huo utaimarisha zaidi nguvu kazi ya walimu.



Naibu Waziri wa Fedha wa zamani, Janeth Mbene (wa pili kulia), akiangalia maonyesho ya vitabu kwenye kongamano la kitaaluma la Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), chuoni hapo Mikocheni jana, kuelekea mahafali ya 21 ya chuo hicho yanayofanyika leo Jumamosi **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wahitimu HKMU watakiwa kufanya utafiti

**Na Joseph Mwendapole**

WAHITIMU wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki (HKMU), wametakiwa kutumia elimu waliyoipata kufanya utafiti na kutatua changamoto mbalimbali zilizoko kwenye jamii

Naibu Waziri wa Fedha wa zamani, Janeth Mbele, alisema hayo juzi wakati wa mjadala kuhusu masuala ya biashara na uchumi kuelekea mahafali ya 21 ya chuo hicho yanayofanyika leo.

Alisema wanapomaliza shahada au stashahada kwenye udaktari, uuguzi au ustawi wa jamii, wasione wamefika mwisho badala yake waendelee kutafuta fursa zikiwamo za ujasiriamali.

Mbene alisema vyuo vinatoa wahitimu wengi lakini soko la ajira ni dogo, hivyo wanapaswa kuwa wabunifu kwa kutafuta mbinu za kujiajiri wenyewe na kuajiri wenzao kwa kutumia ujuzi walionao.

Alisema pamoja na changamoto za huduma za kiafya zinapaswa kuwa fursa kwa na kwenye changamoto nyingi ndiko kwenye fursa hivyo waaanzishe huduma za afya na kuanzisha biashara za huduma hizo.

"Wahitimu wawe wabunifu watoe suluhisho kwa changamoto hizo kwa kuanzisha shughuli mbalimbali ambazo zitaleta suluhisho na tatizo haliwezi kuwa mtaji kama wengine ambao wamekuwa wakitoa visingizo," alisema.

Aliwataka pia kujiendeleza kiteknolojia kwa kuanzisha huduma za kisasa ambazo mara nyingi huwa hazipatikani hasa maeneo ya vijijini hususan kwenye huduma za afya.

"Kama ni daktari, muuguzi unaweza kutumia ujuzi wako kwa kutumia teknolojia kuwahudumia wananchi walioko pale na uwe tayari kujituma kwasababu huduma hizi ni za wito isiwe tu ni ajira uwe na shauku ya kuwahudumia wananchi.

"Ndiyo maana wakati mwingine daktari au muuguzi anaitwa saa nane usiku anakwenda kuwahudumia wagonjwa kwasababu ana wito na kazi yake," alisema.

Mbene aliipongeza HKMU kwa kuanzisha programu atamizi kuwasaidia wahitimu kuanzisha na kuendeleza biashara zao badala ya kutegemea fani zao pekee.

Alisema wahitimu wanapaswa kutumia fursa zilizopo na washirikiane na wenzao kufanya jambo kwa pamoja kwakuwa kwa kufanya hivyo, wanaweza kuona matokeo mazuri mapema kuliko kila mtu kuwa kivyake vyake.

"Nimewapa changamoto wakenye amsuala ya ubunifu kwasababu kwenye mataifa mengi yaliyoendelea wahitimu wao wanakwenda kubuni vitu sasa na watanzania nao wafanye waache visingizo kwamba fursa ni chache watumie mazingira yaliyopo kutengeneza fursa," alisema.

Kuhusu mikopo ya elimu ya juu, Mbene aliitaka serikali kuwa makini na kuhakikisha wanaopewa mikopo hiyo ni wale wanaostahili kwani kumekuwa na malalamiko kwamba watu sahihi wanakosa na wanapewa watu wasiostahili.

"Haya malalamiko mmeyasikia kwa hiyo mimi ninachoweza kusema ni kwamba serikali iwe makini ili wanaopata wawe kweli wale wanaostahili kupata kwasabbau wakipata wenye uwezo inakuwa haina maana," alisema.

## Mpango waanza wa kuchunguza magonjwa mlipuko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA ya Afya kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Mzumbe (MU), imeanzisha mpango wa kuchunguza milipuko ya magonjwa na kufanya ukaguzi wa ubora wa taarifa za magonjwa mbalimbali.

Mradi huo wa kuimarisha mifumo endelevu ya sekta ya afya unafadhiliwa Kituo cha Serikali ya Marekani cha Kukinga na Kudhibiti Magonjwa (US CDC).

Msimamizi mshauri wa Mradi, Dk. Mackfallen Anasel, aliyasema hayo mjini hapa juzi katika kikao kazi cha kutathmini mafanikio yaliopatikana na kuweka mkakati uendelevu wa programu hiyo.

Alisema mradi huo umelenga kuimarisha mafunzo ya Epidemiolojia (FETP) katika ngazi mbalimbali, ikiwamo mafunzo ya ngazi ya awali hadi ngazi ya juu.

Dk. Anasel alisema toka programu hiyo ilipoanza, kuna wahitimu 1,015 ambao wanatoka katika mikoa mbalimbali Tanzania ambao jukumu lao kuu ni kushughulikia ufuatiliaji na kuchunguza milipuko ya magonjwa na kufanya ukaguzi wa ubora wa taarifa za magonjwa mbalimbali.

Alisema hivi karibuni wahitimu hawa walishiriki katika uchunguzi wa mlipuko wa ugonjwa mpya wa Marburg ambao uliwasumbua wananchi waliokuwa wakiharisha damu na kuishiwa nguvu katika eneo la Kagera Machi, 2023.

Kutokana na matokea chanya ya mkakati huo, alisema chuo kikuu kupitia mradi huo kinaomba serikali kutoa kipaumbele cha ufadhili kwa watumishi kada ya afya ili kuendelea kutoa mafunzo hayo na kuendelea kutumia ujuzi wao kikamilifu.

"Eneo lingine la kipambele ni kuimarisha elimu kwa njia ya masafa ili kuwajengea uwezo wataalamu mbalimbali wa afya nchini," alisema. Alisema katika miaka mitatu ya mradi huu, zaidi ya watumishi 40,000 wamefikiwa kupitia mpango wa mafunzo wa ECHO na mfumo wa elimu kwa njia ya masafa ulio chini ya Wizara ya Afya.

"Katika eneo hili Chuo Kikuu Mzumbe , kupitia mradi huu tunaomba serikali kuendelea kuwekeza katika vifaa na miundombinu ya mtandao katika vituo vya afya ili kuwafikia watumishi wengi zaidi,"alisema Dk. Anasel.

Baadhi ya wanufaika na mradi huo, Richard Lupeja na Veronica Donald, walisema fursa ya kushiriki kwenye mafunzo hayo imewasaidia kuongeza ujuzi na maarifa ya ukusanyaji wa taarifa kutoka ngazi ya halmashauri ambako jamii inakabiliwa na changamoto kubwa ya milipuko wa magonjwa ya kuambukiza.

Richard Lupeja alisema awali alikuwa na uelewa mdogo katika ukusanyaji wa taarifa pindi inapotokea jamii inakabiliwa na magonjwa ya mlipuko.





# TAMISEMI yaongoza tuhuma za rushwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) imesema Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mkoani hapa inaongoza kwa malalamiko ya rushwa kwa asilimia 32, ikifuatiwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye asilimia 11.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, John Joseph, wakati akitoa taarifa ya robo tatu ya mwaka ya utekelezaji wa kazi zao mkoani hapa.

Joseph alisema sekta binafsi zinalalamikiwa kwa asilimia tano, ardhi 15, afya 13, Jeshi la Polisi nne, kilimo tano, ununuzi tatu, ujenzi moja na maji nne.

Zingine ni nishati moja, mifugo moja, ajira mbili, baraza la kata moja, maendeleo ya jamii mbili, mahakama tatu, maliasili na utalii mbili, vyama vya siasa mbili, ushirika moja, utawala nne na uvuvi moja. Alisema kipindi cha Oktoba hadi Novemba, 2023 moja ya vipaumbele vya utekelezaji wa majukumu katika taasisi hiyo ni kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Ili kuziba mianya ya rushwa na ufujaji unaoweza kujitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kufuatilia miradi ya ujenzi wa madarasa," alisema. Joseph alisema wamefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo 64 katika mkoa huo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 27.7 na kubaini baadhi ina mapungufu ya miradi 28 yenye thamani ya zaidi Sh. bilioni 5.16.

Alisema ufuatiliaji umefanyika katika elimu miradi 51, ujenzi mmoja, afya mitatu, maji mitano, utawala mmoja, ustawi wa jamii mmoja na mifugo miwili.

Alitaja upungufu katika miradi mingi kuwa ni pamoja na majengo kutumia mabati yaliyo chini ya kiwango, baadhi kuwa na nyufa na wazabuni kulipwa fedha kabla ya kuwasilisha vifaa na kupeleka mapungufu eneo la ujenzi. Kasoro zingine ni fedha za zuio kukatwa kwa makandarasi na kutowasilishwa katika mamlaka husika na kupelekea kufunguliwa majalada ya uchunguzi kwa baadhi ya miradi. Alisema katika kutekeleza programu ya TAKUKURU rafiki kwa kushirikiana na wadau kutoka kwenye sekta mbalimbali, imezifikia kata 18 mkoani hapa na kuibua kero 130 kutoka sekta za elimu, afya, ardhi, mifugo, maji, utawala, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Polisi na kuzipatia ufumbuzi.

Vilevile, alisema TAKUKURU mkoani hapa imepokea malalamiko 165, kati ya hayo, 112 kuhusu rushwa na kufungua majalada ya uchunguzi, 12 umekamilika na matano yamewasilishwa katika ofisi ya mashtaka kwa hatua zaidi na mengine matano vibali vya kufungua mashauri vimetolewa.

# BAKWATA watakiwa kuwa wabunifu zaidi

**Na Peter Mkwavila**,
DODOMA

VIONGOZI wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma wametakiwa kuwa wabunifu kwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali ili kuwasaidia wajane, yatima na wazee na wasiojiweza.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkufunzi Mkuu wa BAKWATA Online Academy (BOA), Ally Amani Ally, wakati wa semina elekezi kwa viongozi wa baraza hilo wa mikoa, wilaya, kata, makatibu, wahasibu na wajumbe iliyofanyika Msikiti Mkuu wa Gadaff jijini hapa.

Ally aliwataka viongozi hao kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kujitambua kama wanavyoelekezwa na Mufti Mkuu wa Tanzania, Abubakary Zuberi.

Aliwataka kuongeza maarifa kwenye utawala bora, kutambua, kupanga, kuratibu, kuongoza na kudhibiti mambo yasiyofaa ili kuwaunganisha Waislamu nchini.

Ally alisema miradi ikianzishwa ndani ya misikiti itasaidia kukuza uchumi na kubadilisha maisha ya waumini wa dini hiyo.

Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Alhaji Bashiru Omary, alisema semina hiyo itasaidia kuwabadilisha viongozi hao katika utendaji wao.

"Bado kuna viongozi ndani ya BAKWATA walio na muda mrefu na wale wenye muda mfupi kwa maana hiyo semina kama hii itawawezesha kufanya kazi kwa ufanisi," alisema




Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata (kushoto), akikabidhi tuzo ya mlipakodi mkubwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa M.M . Integrated Steel Mills Ltd (MMI), Veer Patel (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Ratish Kamania wakati wa hafla ya utoaji tuzo za walipakodi wa mwaka 2023, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madiwani wawatimua watumishi kwa ulevi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, limewafukuza kazi na kuwasimamisha watumishi wanane kwa tuhuma za kushindwa kutekeleza majukumu na ulevi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, James Mkwega, alikiambia kikao cha baraza hilo juzi wakati wa kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha wa 2023/24.

Aliwataja watumishi hao kuwa ni mtabibu msaidizi na muuguzi wa zahanati za halmashauri hiyo.

Makwega alisema watumishi hao wamepewa adhabu hiyo kwa kosa la utoro kazini kwa zaidi ya siku tano bila kutoa taarifa kwa mwajiri.

Aliwataja watumishi wawili waliopewa adhabu ya kukatwa mshahara kwa asilimia 15 kwa miaka mitatu kutokana na ulevi uliokithiri ni ofisa manunuzi msaidizi na mteknolojia mwandamizi wa maabara .

Watumishi wengine walipewa barua ya onyo kwa kosa la kukiuka taratibu za fedha na manunuzi ni ofisa mtendaji wa kijiji na mteknolojia wa dawa kituo cha afya.

Mwingine ni mtabibu msaidizi ambaye alikuwa akituhumiwa kwa ulevi, baraza limeamuru tuhuma dhidi yake kuchunguzwa upya.

Akizungumza baada ya kusoma maamuzi ya baraza hilo, alisema madiwani hawafurahii kumwita mtumishi kwenye kamati ya uongozi kuhojiwa kwa tuhuma za ulevi.

Aliwataka watumishi kuzitendea haki nafasi zao kwani wapo watu ambao wameenda kwa waganga wa kienyeji na wengine kuombewa ili wapate nafasi za kuteuliwa, lakini hawakufanikiwa.

"Mwaka 2014/2015 haikutokea kujadili mtumishi yeyote kwenye kamati ya uongozi, lakini leo hii inatokea mtumishi anajadiliwa kunywa pombe halafu pombe kwanza haijakatazwa kunywa kinachotakiwa usinywe wakati wa kazi," alisema.





# Walimu masomo sayansi wanolewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imeanzisha kozi maalumu ya diploma kwa ajili ya kukabiliana na uhaba wa walimu masomo ya sayansi katika shule za sekondari visiwani hapa.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ali Abdulghulam Hussein, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu, Fatma Ramadhan Mandoba katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliyetaka kujua mikakati ya wizara kuzalisha walimu wa masomo ya sayansi.

Hussein alisema wizara hiyo imeanzisha kozi hizo kwa walimu ya miaka miwili na kuzalisha walimu 524 wa masomo hayo.

Alisema kupitia washirika wa maendeleo katika sekta ya elimu, wanatekeleza mradi wa kusaidia kuinua kiwango cha elimu kwa walimu wa sayansi.

Naibu waziri huyo alisema wizara hiyo ipo katika hatua za mwisho za kurudisha chuo cha ualimu kitakachotoa mafunzo ya walimu na mbinu zake.

Alisema upembuzi yakinifu umeanza kufanyika ikiwa ni pamoja na kutayarisha michoro ya ujenzi wa jengo ambalo litatumika kufundisha walimu mbinu za kufundishia.

"Mheshimiwa Spika nataka niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi na walimu wa masomo ya sayansi hatua ambayo tunaamini itasaidia kuzalisha walimu zaidi," alisema.

Alisema wizara hiyo ipo katika hatua za mwisho za ujenzi ya maabara 10 za sayansi kusaidia kukuza vipaji vya wanafunzi katika masomo hayo.

Alisema ujenzi wa maabara hizo katika baadhi ya shule umekamilika ikiwemo katika Kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja.

"Tunajenga shule 10 zikiwa na maabara ya masomo ya sayansi ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuzalisha walimu wa masomo hayo hatua ambayo itawawezesha wanafunzi wetu kuingia katika ushindani wa ajira," alisema.

# Sheria Mahakama ya Kadhi yafutwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha kufutwa kwa sheria ya Mahakama ya Kadhi visiwani hapa na kuanzisha mpya itakayoipa nguvu kuvunja ndoa na mgawanyo wa mali kati ya mke ma mume.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha baraza hilo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akifanya majumuisho ya michango iliyotolewa na wajumbe baada ya muswada huo kuwasilishwa.

Alisema sheria hiyo mpya ya mwaka 2023 baada ya kuifuta sheria hiyo namba 9 ya mwaka 2017, itakapoanza kutumika itaondoa mivutano ya mgawanyo wa mali pindi wanandoa wanapotengana.

Waziri alisema kabla ya sheria hiyo kuvunjwa ni kutungwa mpya, wanandoa walipokuwa wakiachana, malalamiko zaidi yalikuwa kwa wanawake kutokana na kutoridhishwa na mgawanyo wa mali.

Haroun alisema kwa mujibu wa marekebisho hayo, mgawanyo wa mali baada ya kufungwa kwa ndoa utatambuliwa rasmi na kupigiwa hesabu.

Alisema mali iliyochumwa kabla ya kufungwa kwa ndoa, haitaingizwa katika mgawanyo kwa wanandoa na kupigwa thamani yake.

Muswada huo, alisema umewasilishwa kwa lengo la kuundwa upya kwa mahakama hiyo katika utekelezaji wa majukumu, kuleta ufanisi na uwajibikaji kwa wananchi.

Alisema muswada huo unakusudia kuimarisha mfumo wa utoaji wa haki katika ngazi mbalimbali na kupendekeza masharti yanayowatambua wabobezi katika sheria za Kiislamu.

Aliyataja baadhi ya maboresho makubwa katika mahakama hiyo ni kuwepo kwa watendaji wenye viwango vya elimu kuanzia shahada ya kwanza katika sheria za Kiislamu.

Katika maboresho hayo, mahakama hiyo imeongezewa uwezo wa kutoa amri tofauti na awali wananchi wengi walikuwa wakipuuza amri zake.

"Tumefanya marekebisho makubwa katika Mahakama ya Kadhi ambayo sasa ni sawa na mahakama nyingine katika kutoa maagizo yake na amri ya wito na kukamata," alisema.

Historia ya Zanzibar inaonyesha mahakama hiyo ni taasisi kongwe iliyoanzishwa wakati wa utawala wa Sultani wa Oman katika mfumo usiokuwa rasmi wa sheria mwaka 1832.

Kabla ya kuanzishwa kwa mahakama hiyo, jamii ilikuwa ikitatua matatizo kupitia viongozi wa Kiislamu.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT), Charles Ogutu akizungumza na wadau wa kilimo (hawapo pichani), wakati wa ufungaji wa kongamano la siku tatu la kujifunza na kubadilishana uzoefu, lililoandaliwa na taasisi hiyo jijini Dodoma hivi karibuni. Kongamano hilo lilihudhuriwa na zaidi ya washiriki 100 kutoka ndani na nje ya nchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZEC yaanza uboreshaji daftari la wapigakura

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) leo inatarajia kuanza rasmi uboreshaji wa daftari la wapigakura kwa awamu ya kwanza katika wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mpango huo na matayarisho ya uandikishaji wa wapigakura wapya katika daftari hilo litakalotumika katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2025.

Akizungumza jana kisiwani Pemba na watendaji wanaotarajiwa kufanya kazi hiyo, Mkuu wa Kurugenzi ya Mifumo ya Uchaguzi ZEC, Mwanakombo Machano Abuu, aliwataka kufanya kazi kwa mujibu wa haki na malengo yaliyokusudiwa.

Mwanakombo alisema watendaji hao wanapaswa kutambua kuwa jukumu hilo ni la kitaifa, hivyo linahitaji kuendeshwa kwa weledi na kutimiza malengo ya taifa kupitia mfumo wa kidemokrasia.

"Zoezi la uandikishaji halihitaji ushabiki wa kisiasa. Niwaombe sana jiepusheni kushabikia vyama wakati wa uandikishaji kutatia dosari zoezi zima.

"Niwatake kila mmoja wenu aelekeze akili yake katika kazi hiyo kwa kuzingatia haki na sheria bila kujali mtu anatokea chama gani," alisema.

Aliwataka kutoa vipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalumu ikiwemo wazee, wajawazito, watu wenye ulemavu ili wapate haki hiyo bila usumbufu.

Mkuu wa Kurugenzi ya Huduma kwa Wapigakura ZEC, Salum Juma, aliwataka watendaji hao kuwa makini katika utunzaji wa vifaa vya uandikishaji na kuepuka kuchezea mifumo ya kuandikia.

"Kama tunavyojua zoezi hili la uandikishaji mara hii ni la kidigitali zaidi kwa hiyo mnatakiwa vifaa tuvitunze vizuri ili vitumike mara nyingi zaidi katika uandikishaji," alisema. Ofisa Uandikishaji wa ZEC Wilaya ya Mkoani, Juma Fumu Makame, alisema lengo la mafunzo hayo kwa wakuu wa vituo na makarani ni kuwapa ujuzi utakaosaidia kufanikisha zoezi hilo kwa umakini zaidi.

Aliwataka wananchi wenye sifa za kuadikishwa katika daftari hilo kujitokeza ili kutumia haki yao ya msingi katika ushiriki wa demokrasia ya uchaguzi.



**NAIRA MARLEY AONEKANA HADHARANI** Uk. 14





# Tabu iko palepale

KILICHOMPATA mwanamuziki wa R&B wa Marekani, R.Kelly ambaye anatumikia kifungo cha miaka 30 jela, ndicho kinaweza kumpata rapa mkongwe Sean Combs kutokana na tuhuma zinazowakabili kufanana.

Combs ambaye anajulikana kama Diddy yuko katika wakati mgumu baada ya kuandamwa na mashtaka mazito ya unyanyasaji wa kingono.

R Kelly alianza kama ilivyo kwa Diddy, kwani mwanamke mmoja alianza kujitokeza akidai kunyanyaswa kingono, kabla ya msururu wa wanawake wengine kujitokeza wakidai nao kufanyiwa vitendo hivyo vya kikatili.

Kwa upande wa Diddy, aliyeanza kumshtaki ni mpenzi wake wa zamani Casandra Ventura, maarufu kama Cassie, ambaye walimalizana kwa kulipa kitita kikubwa cha pesa katika usuluhishi uliofanywa nje ya mahakama.

Kutokana na kuongezeka kwa tuhuma hizo, Diddy, aliamua kujiuzulu kama mwenyekiti wa kampuni ya habari ya Revolt TV ili kukabiliana na matatizo hayo.

Kulingana na taarifa hiyo Sean Combs amejiuzulu kutoka nafasi yake kama mwenyekiti kwa sababu anataka kuweka dhamira ya kuunda maudhui kwa utamaduni na kukuza sauti za watu weusi wanaoishi Marekani na nje ya Afrika.

Combs amekuwa akikabiliana na kesi tatu za unyanyasaji ikiwamo ubakaji na kuwapiga wanawake na kuwasababishia madhara ya kiakili.

Wiki moja baada ya kesi ya kwanza, Joi Dickerson-Neal alimshtaki rapa huyo akidai kwamba alimnywesha dawa za kulevya na kumbaka mwaka wa 1991.

Kesi ya tatu imewasilishwa na mlalamikaji aliyejulikana kama Jane Doe, ambaye anadai kuwa Diddy na msanii wa R&B Aaron Hall walifanya zamu kuwabaka yeye na wanawake wengine katika nyumba ya mwimbaji huyo miaka ya 1990.

Diddy alikuwa amekanusha madai hayo yote, akiyataja kama "madai ya kubuni" na majaribio ya "kunyakua pesa."

BASI SAWA

## ‘Tabulele Remix’ kusikika leo

MKALI wa Bongo Fleva, Harmonize na msanii kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Riger maarufu kama Tabulele, leo watawatumbuiza mashabiki wa klabu ya soka ya Yanga kwa kibao chao kipya.

Dogo huyo kutoka mitaani ameingia studio tangu juzi kuandaa marudio ya wimbo wa ‘Tabulele’ ambao umepata umaarufu katika mitandao ya kijamii.

Hata hivyo Klabu ya Yanga umeufanya kipande cha wimbo huo kuwa kibwagizo cha kuchochea uhamasishaji wa ushindi wa timu hiyo.




## Omondi hataki wapenda bata

MCHEKESHAJI kutoka Kenya, Eric Omondi amewataka watu wenye wazo la kumtumia kuchangisha pesa kwa ajili ya karo za shule na harusi wasithubutu kumfikia, kwa sababu yeye sio mtu wa aina hiyo.

Omondi ambaye amekuwa mstari wa mbele kuchangisha fedha kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye matatizo mbalimbali, amesema yeye huguswa na wale wanaopata shida za kiafya na ugumu wa maisha pekee.

“Siongozi michango ya karo za shule au harusi, ninachangia watu ambao wanategemea pesa hizo kwa maswala mazito. Ukigusa hizo pesa, unaweza kulaaniwa. Tunashughulika na matatizo kama upandikizaji wa figo, mtu ambaye mwanawe yuko ICU na mengine mazito,” amesema.





## D Voice ajishangaa kwa kupanda thamani

MWANAMUZIKI mpya wa lebo ya muziki ya WCB, D voice, amesema hata yeye anajishangaa jinsi siku chache kuwa na mabadiliko makubwa ikiwamo kuvaa mavazi na mapambo ya gharama kubwa.

D voice amesema hata siku moja hakutarajia kuvaa mikufu ya mamilioni ya pesa, lakini bosi wake Diamond Platnumz amemfanya kuwa na mtazamo mpya kutokana na kumpa vitu hivyo kama zawadi yake.

“ Diamond ni msanii ambaye anapenda kushirikiana na wafanyakazi wake vyema, mimi ni mmoja wao ambaye nilishangaa kuona jinsi alivyo mkarimu baada ya kunikabidhi pete mbili za dhahabu zenye thamani ya Sh 42,000,000,” amesema.





## Baba levo kalichokoza

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Baba Levo, amesema Diamond Platnumz ndiye msanii pekee hapa nchini anayeagiza magari kiwandani kwa ajili ya matumizi yake.

Amesema wasanii wengi magari yao wanayoyatumia kwa usafiri wamenunua kama mitumba, hivyo wanapoonekana wanaringa na kumsema mitandaoni huwa anawashangaa.

“Magari yote wanayotumia wasanii hapa nchini yametumika Japan, hakuna anayeweza kununua kutoka kiwandani isipokuwa Diamond Platnumz

pekee ambaye ndiye mwenye uwezo wa kutoa oda ya kutengenezewa gari,” amesema

## Wamepiga zote, Msondo na Sikinde

**Na Adam Fungamwango**

KAMA zilivyo Simba na Yanga kwenye soka, kwenye mambo ya muziki nchini kuna utani wa jadi au upinzani katika bendi mbili kubwa kabisa.

Bendi hizi ni Msondo Ngoma Music Band na Orchestra Mlimani Park, ikitumia mtindo wa Sikinde Ngoma ya Ukae.

Ni bendi zenye mashabiki wengi nchini waliogawanyika pande mbili kama zilivyo timu za mpira wa miguu za Simba na Yanga.

Kila upinzani una historia yake. Msondo ilianzishwa mwaka 1964 na Chama cha Wafanyakazi Tanzania na kuiita NUTA Jazz Band, ikitumia mitindo mbalimbali na baadaye Msondo Ngoma.

Ilikuwa ikibadilisha majina ya bendi kulingana na siasa za nchi, hasa Chama Cha Wafanyakazi kilivyokuwa kikijibadilisha majina.

Upinzani wao na Sikinde ulianza mwaka 1978, baada ya baadhi ya wanamuziki wa Msondo wakiongozwa na Muhidini Mwalimu Gurumo na kwenda kuanzisha Mlimani Park Orchestra.

**Muhidini Mwalimu Gurumo**

Alikuwa mmoja wa viongozi wa Juwata Jazz, lakini aliondoka mwaka 1978 na kwenda kuunda Sikinde. Na ni mmoja wa wanamuziki waliosababisha upinzani mkubwa kati ya bendi hizo mbili.

Gurumo ni nembo ya bendi zote hizo mbili kwani hata majina ya Msondo na Sikinde ni yeye ndiye aliyeyabuni.

Alirejea tena Msondo mwaka 1990 na hakuhama tena hadi alipofariki 2014 akiwa na miaka 74.

**Hassan Rehani Bitchuka**

Awali alikuwa mwimbaji tegemeo wa sauti ya kwanza kwenye bendi ya Msondo Ngoma.

Hata alipohama Gurumo mwaka 1978, Msondo ilionekana kutotetereka kwa kutoa vibao vingine vikali kama ‘Sogea Karibu’ na ‘Uzuri si Shani’.

Hata hivyo, Sikinde iliwapa pigo Msondo mwaka 1979, ilipomchukua Bitchuka na kuacha kilio kikubwa.

Baada ya miaka 11, Bitchuka alirejea tena Msondo akiwa pamoja na swahiba wake Gurumo.

**Shaaban Dede**

Baada ya kuhangaika kwa muda mrefu kumpata mtu atakayeweza kufanana sauti na Bitchuka, hatimaye Msondo walimpata mwimbaji wa aina hiyo kutoka Dodoma International, Shaaban Dede.

Huyu alituliza kidogo mizuka ya mashabiki wa Msondo Ngoma kutokana na sauti yake kuwa na mfanano na Bitchuka.

Hiyo ilikuwa mwaka 1979. Lakini kama kawaida ya Sikinde. Huenda ilikuwa ina mikakati ya kuidhohofisha Msondo, kwani mwaka 1982 ilimchukua pia Dede na kuwaacha viongozi na mashabiki wa Msondo wasijue la kufanya.

Alirejea tena Msondo mwishoni mwa miaka ya ‘80, na kutunga nyimbo kama ‘Sauda’ na ‘Kimwaga.’

**Fresh Jumbe**

Akitokea Tanga, alichukuliwa na Marijan Rajab kwenye bendi ya Dar International, lakini muda mfupi tu akanyakuliwa na Msondo Ngoma. Hiyo ilikuwa ni miaka ya ‘80.

Akaingia na vibao kama ‘Ama zake Ama zangu’ na ‘Pamela’ zilizompa umaarufu mkubwa.

Mwishoni mwa miaka ya ‘80 alichukuliwa na Sikinde.

Huyu naye anaingia kwenye orodha ya wanamuziki waliowahi kupigia bendi hizo mbili hasimu.

**Suleiman Mwanyiro**

Ni mpiga besi ambaye awali alikuwa akipiga kwenye bendi maarufu za taarabu Tanga, Black Star na Lucky Star.

Alichukuliwa na Msondo miaka ya ‘70 na kufanya kazi kwa umahiri mkubwa hadi alipokuwa mmoja wa wanamuziki walioihama bendi hiyo na kwenda Sikinde.

Naye pia alikuwa mmoja na mlolongo wa wanamuziki waliokuwa wakihama na kurejea tena, kwani miaka ya 2000 alirejea tena Msondo na kutunga vibao vikali kama ‘Kauka Nikuvae’, ‘Sekuntoza Kigudi Chauma’, ‘Tuelewane Mke wangu’ na nyingine nyingi, kabla ya kuelekea tena Sikinde. Alifariki mwaka 2004.






## Timu mbovu: Mashabiki wanahama

**Na Adam Fungamwango**

‘TIMU Mbovu’ ni filamu inayozungumzia mambo yanayozikumba baadhi ya ndoa kwenye jamii.

Watu wanaweza kuoana, wakiwa wazima, lakini baadaye mmoja akapata ugonjwa mambo ya ndoa yakawa yameishia hapo.

Wapo baadhi ya wanaume huwa ni wagonjwa tangu zamani lakini wanaoa tu kwa sababu na wao waonekane ni wazima na kupata heshima kwenye jamii, lakini wakati mwingine si hivyo, wanapata wakati mgumu, fedheha na aibu.

Imesemwa na kina, Tin White, Siri Mohamed, Rehema Abdallah, Abdallah Nzunda ‘Mkojani’, na wengineo.

Picha linaanza kwanza mpangaji mmoja anaitwa Tuti, anamfuma mwanaume wa nyumba ya jirani aitwaye Baba J akitoka kwenye chumba cha Mkojani.

Tuti anamuonya Baba J, tabia ya kutembea na mke wa Mkojani kwani ni mke wa mtu wakati pia na yeye ni mume wa mtu.

Baadaye Tuti anahamishwa kwenye nyumba hiyo. Kumbe pia mke wa Mkojani, Angel ana mwanaume mwingine wa nje, naye ni Tin White. Naye pia ni rafiki wa Mkojani ingawa hawakai  jirani.

Siku moja, mke wa Mkojani anamuaga mumewe kuwa anakwenda kwa mama yake na atakaa kwa siku tatu. Mkojani anatoa ruhusa. Upweke unamsumbua Mkojani, hivyo kesho yake akaamua kwenda kwa rafiki yake Tin White kumsalimia.

Anakutana naye njiani. Anaanza kusifia kuwa nyumbani kwake ana mpenzi mzuri sana ambaye alifika jana. Lakini akamwambia pia ni mke wa mtu.

Kwa bahati mbaya pamoja na kujuana, alikuwa hamjui mke wa Mkojani. Wakafika nyumbani kwake. Kwa macho yake Mkojani akamuona mkewe. Kumbe hakwenda kwa mama yake, alikwenda kwa Tin White. Akazimia. Alipozinduka kesi ikawa serikali za mitaa.

Baada ya yote kuzungumzwa na Tin kubebeshwa kosa la kuchukua mke wa mtu, Angel aliwaambia wajumbe kuwa anataka talaka yake pale pale ili ahamie kwa Tin kwa sababu mumewe timu yake ni mbovu, kwa hiyo yeye kama shabiki anahama. Akiwa na maana kuwa mumewe hamna kitu ndani, ‘nyumba haina umeme.’

# Mwacheni Beyonce ang'are



MAMA mzazi wa mwanamuziki nyota wa Marekani, Beyonce Knowles, amekuwa mkali baada ya watu kumsakama mtoto wake huyo kuwa ngozi yake imepauka kutokana na kuwa na tabia ya kujichubua.

Tina Knowles ambaye amekuwa mara kwa mara akijitokeza kumtetea binti yake, amesema kinachofanyika sasa ni wivu na ubaguzi wa rangi unaofanywa na baadhi ya watu.

Uvumi kwamba Beyonce anatumia madawa ya kubadili mwonekano wa ngozi yake, uliibuka baada ya picha zilizosambaa za onyesho lake la kwanza la Renaissance kuonekana ngozi yake imepauka.

Knowles aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa madai kwamba mtoto wake anajichubua ni wivu na chuki iliyopitiliza na ni sawa na tendo la kibaguzi.



## Oladips kama si kweli mbona unakuwa mkali?

RAPA aliyejizolea umaarufu katika mitaa ya watu maskini nchini Nigeria, Oladips amekanusha madai kwamba alijizushia kifo kwa ajili ya kutangaza albamu yake mpya inayoitwa Superhero Adugbo.

Oladips amemlalamikia msanii mwenzake Qdot kwa kuibua hisia hizo ambazo hazina ukweli.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Oladips amesema yeye na Qdot hawajazungumza kwa muda wa mwaka mmoja, uvumi huo kwenye mitandao ya kijamii uliwekwa kwa makusudi ili kumvunja moyo.

## Naira Marley aonekana hadharani

STAA wa muziki wa Afrobeats kutoka Nigeria, Naira Marley, na rafiki yake wa karibu, Sam Larry, wameonekana hadharani kwa mara ya kwanza tangu watoke mahabusu kwa dhamana.

Wawili hao wanatuhumiwa kuhusika na kifo cha mwanamuziki Mohbad na walitoka kwa dhamana ya Naira milioni 20 baada ya kurejeshwa na mahakama.

Katika video hiyo ya mtandaoni iliyotumwa kupitia mtandao wa TikTok, ameonekana Larry na Marley, na msanii mwingine Zinoleesky, wakitembea kwenye mitaa.





## Iyanya atoa ushauri kuimarisha ndoa

MWANAMUZIKI maarufu, Iyanya, amewashauri wanandoa kuacha kutumia muda mwingi kwenye mitandao ya jamii.

Iyanya amesema kuwa anaamini ndoa ni kitu kitakatifu na kizuri bila kujali mabaya na kusisitiza umuhimu wa kuilinda dhidi ya watu wabaya.

"Nawafahamu watu walio kwenye ndoa si kwamba hawana changamoto bali wanalinda walichonacho. Lazima ulinde ndoa kwani haipo kwenye Instagram," amesema.

## Tonto ampa makavu baba wa Mohbad

MWIGIZAJI maarufu kutoka Nollywood, Tonto Dikeh, amemjia juu baba mzazi wa mwanamuziki Mohbad ambaye kifo chake kimeibua utata, akieleza ana tamaa na mali na pia ana nia ya kumdhulumu mtoto wa marehemu.

Dikeh alichapisha picha ya marehemu Mohbad katika mtandao wa Instagram na kuambatanisha na maneno makali kwa baba yake na kueleza kukerwa na kile anachokiona kama tamaa iliyopitiliza kwa mzee huyo.

Aidha alilaani mazishi ya haraka yaliyofanywa na familia, kabla ya watu kupiga kelele na hatimaye kufukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi kujua chanzo cha kifo chake.





# Waomba msaada kulea mapacha wanne

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKAZI wa Kwamorombo jijini hapa, Janeth Manota (27), amewaomba Watanzania msaada wa kuwalea watoto mapacha wanne wa kiume kutokana na uwezo wake mdogo kifedha.

Akizungumza na Nipashe katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, alisema amejifungua mapacha hao Novemba 26, mwak huu, kwa njia ya upasuaji wenye afya njema wakiwa na uzito wa kilogramu 1.4, 1.5, 1.8 na 1.9.

Manota aliishukuru hospitali hiyo kwa kumpatia huduma nzuri na kumwezesha kujifungua watoto hao salama ikiwa ni uzao wake wa pili, ukitanguliwa na mtoto wake wa kiume mwaka 2015. Alisema akiwa na ujauzito wa mapacha hao kuanzia miezi minne, alikabiliwa na changamoto kubwa ya kuishiwa na damu, maumivu ya mgongo, kichwa na kulazimika kupumzishwa kitandani hadi siku ya kujifungua.

"Pamoja na kwamba nimejifungua salama, sijui nitawalea kwa namna gani sababu uwezo wa kiuchumi nilio nao ni mdogo katika familia yangu. Naomba Watanzania wanisaidie ili kuwalea vizuri, ikiwamo huduma ya maziwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema serikali ya wilaya imeanza kuchukua hatua ya kumsaidia mzazi huyo namna ya kulea watoto hao, ikiwamo kuwakatia bima ya afya na wadau wameonyesha nia ya kuunga mkono jitihada hizo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Alex Ernest, alisema Novemba 26, mwaka huu, majira ya saa 9:00 usiku, Manota alijifungua kwa upasuaji mapacha hao wakiwa na afya njema.

Alisema suala la kujifungua mapacha wengi ni la kawaida na hutokea kwa nadra kulingana na historia za koo, familia au changamoto za uzazi.

Hospitali hiyo, alisema inawapa kipaumbele wajawazito wakati wa kujifungua bila kudaiwa chochote ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa serikali wa kupunguza na kuondoa vifo vya wajawazito nchini.

Crey Julias, alimshukuru Mungu kwa mkewe kujifungua salama watoto hao na kuwaomba Watanzania kumsaidia kuwalea watoto hao kwa sababu kipato chake anachopata kwenye vibarua vya ujenzi ni kidogo.

Alisema pamoja na kuelemewa na mzigo wa kuwalea mapacha hao, bado ana hamu ya kuendelea kupata watoto wengine.



Kansela wa Ushirikiano na Maendeleo wa Ubalozi wa Canada nchini Tanzania, Hellen Fytch (katikati-aliyeweka mikono mfukoni), akisikiliza ushuhuda wa kiongozi wa mila, Furanael Nnko (hayupo pichani), ambaye ni mnufaika wa mradi wa kukuza usawa kwa kutumia elimu ya haki za binadamu, unaotekelezwa na Shirika la TUSONGE, linalofadhiliwa na Serikali ya Canada, kupitia Kituo cha Elimu cha Kimataifa cha EQUITAS, wakati wa hafla ya kufunga mradi wa haki za binadamu, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# TAKUKURU yaagizwa kuwakamata makandarasi wanaohusika na rushwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imeiagiza Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) kuwachunguza na kuwachukulia hatua makandarasi wazawa wanaojenga miradi chini ya kiwango kwa kujihusisha na rushwa ili kukomesha tabia ya kulichafulia sifa taifa.

Vilevile imeilekeza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) kuangalia upya vigezo vya usajili wa makandarasi ili kuongeza idadi ya wanachama kujiunga na Taasisi ya Wahandishi Tanzania (IET). Akifungua mkutano wa 32 wa IET, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, kwa niaba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema inasikitisha kuona wahandisi wazawa wanashindwa kupewa kazi nyingi sababu ya ukosefu uaminifu, uadilifu na kuendekeza rushwa.

"Tujitathimini na tuisaidie serikali kujenga nchi hasa kwenye miradi hii inayotekelezwa maeneo mbalimbali. Hivi sasa tunakabiliwa na miradi mingi inayotekelezwa na baadhi ya wazawa chini ya kiwango, mfano kama barabara inatakiwa idumu miaka 20, inakaa miaka sita inaharibika, huu ni upotevu wa fedha za umma.

""Lazima tuwalaumu nyie makandarasi wazawa kwa kusababisha kazi nyingi ziende kwa watu wa nje. Naomba kampuni zenu zisifanye hivyo na kesi hizo zinajirudia kuweni walinzi wa kwanza wa rasilimali hizi za nchi na hapa nataka TAKUKURU kamateni wanaohusika na ujenzi wa miradi chini ya kiwango ili wawe mfano kwa wenzao," alisema.

Alisema tabia hizo serikali haifurahishwi kutumia asilimia 62 ya fedha zake kulipa makandarasi wa nje huku wazawa wakilipwa asilimia 38.

Waziri huyo alisema wakati ERB ikisajili makandarasi 36,709, waliojiunga na IET 4,900 idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na ya Watanzania ambao ni zaidi ya milioni 61.

"Idadi hii ndogo ukizingatia kila mkandarasi mmoja anatakiwa kuhudumia watu 5,000 na Watanzania tuko zaidi ya milioni 61. Naekeleza tuangalie upya vigezo vya usajili ili kutoa fursa kwa wengine hasa vijana wapya kujiunga bila kuathiri taaluma na kusaidia kujenga nchi yetu kwa pamoja," alisema. Rais wa IET, Dk. Gemma Modu, alishukuru serikali kwa kuongeza kuwapa kazi wahandisi wazawa kwenye miradi mikakati inayoendelea kujengwa nchini.

"Hali hii ikiendelea itasaidia kufungua kiwango cha kazi kwa wahandisi wazawa pamoja na kuwainua kiuchumi na kuongeza ajira kwa wengine, ukizingatia wahandisi wana mchango mkubwa wa kuleta maendeleo endelevu nchini," alisema.

Makamu wa Rais wa IET, Asa Mwaipopo, alisema washiriki wa mkutano huo wa siku tatu ni 800 na wenguine 60 wanafuatilia kwa njia ya mtandao.

Alisema wahandisi 57 wamekula kiapo cha kufanya kazi kwa uadilifu kwa mujibu wa sheria.

# Mbegu feki pasua kichwa

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amewaagiza wananchi na wadau kuwafichua wafanyabiashara wanaouza mbegu feki ili serikali iwachukulie hatua kwa kuwasababishia wakulima hasara.

Sendiga alitoa agizo hilo jana wakati akifungua kikao kazi cha wadau wa mbegu za mazao kilichoandaliwa na Tume ya Ushindani (FCC) Kanda ya Kaskazini.

"Tunaendelea kuwabaini wanaozalisha mbegu feki na hili tulijadili kwa kina na tusifumbie macho wahalifu wanaozalisha mbegu feki," alisema.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wa mbegu ni mtihani kwao kusimamia bei elekezi inayotolewa na serikali wakati wanajua mbegu ni uhai kwa kuwa ni chakula.

Mkuu wa FCC Kanda ya Kaskazini, Nonge Juma, alisema lengo la kikao kazi hicho ni kuhakikisha soko linakuwa na ushindani.

Juma alisema baadhi ya vitendo vilikuwa vinafanywa na wafanyabiashara vya kuongeza bei, kutoingiza mbegu sokoni na kuwa na matangazo yasiyo ya ukweli ambayo maelezo hayaendani na bidhaa husika kwenye vifungashio.

Mtaalamu huyo alisema wanataka soko la mbegu lifanye vizuri na wanaokaidi sheria namba 8 ya ushindani ya mwaka 2003 inayokataza matangazo yasiyokuwa sahihi wachukuliwe hatua kali ikiwemo kutozwa faini.

"Tunatoza faini kulingana na mapato yako ghafi ya mwaka uliopita kwa mujibu wa ripoti ya ukaguzi," alisema Juma.

Mkuu wa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) Kanda ya Kaskazini, Dk. Munguatosha Ngomuo, alisema mbegu zinazonunuliwa na wakulima zinatakiwa kuwa na nembo ya TOSCI ikiwa kwenye mfuko miezi saba kabla ya kuuzwa.

Dk. Ngomuo alisema wafanyabiashara wa mbegu lazima wasajiliwe TOSCI na kupewa mafunzo na kwamba watakaokiuka watakumbana na mkono wa sheria.

Mkuu wa Kitengo cha Mahindi Kituo cha Utafiti Selian, Zabron Msengi, alisema wakulima wanatakiwa kununua mbegu kwa mawakala wanaotambuliwa na serikali baada ya kuhakikiwa na TOSCI na wahifa-

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Yalikotoka majina ya utani ya wachezaji wa Bongo enzi hizo

## -Mensah, Bwalya, Chama, Chukwu...

Na Adam Fungamwango

KILELE cha soka la Tanzania kilikuwa miaka ya 1974 na 1975. Ndipo Bongo ilikuwa na kiwango cha juu kwa ngazi ya klabu ambacho hadi leo hakijafikiwa.

Mwaka 1974 ndiyo ambao Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika kwa kuipita Hearts of Oak ya Ghana.

Kwenye mechi ya kwanza ikiwa ugenini, Simba ilishinda mabao 2-1, ikalazimisha sare nyumbani nchini Tanzania na kufanikiwa kusonga mbele kwa jumla ya mabao 2-1.

Kwa bahati mbaya sana ilitolewa hatua ya nusu fainali na Mehalla El Kubra ya Misri jijini Cairo kwa mikwaju 3-0 ya penalti, baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Hadi leo Simba, au klabu yoyote ya Tanzania haijawahi kufikia hatua hiyo.

Mwaka 1975, Yanga nayo ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Enugu Rangers ya Nigeria. Na hiyo ilikuwa ni mara ya pili baada ya ile ya mwaka 1968 dhidi ya Asante Kotoko mwaka 1969.

Miaka hiyo ya mwishoni mwa 1960, 1970 hadi 1980, timu za Tanzania zililazimika kucheza na timu ngumu za Afrika Magharibi wakati huo, hata za Kusini mwa Jangwa la Sahara kama Zambia, Zimbabwe na Malawi.

Ndiyo kipindi wachezaji wengi mastaa wa Tanzania walipachikwa majina ya wachezaji mbalimbali na timu za nje waliokuwa wakija kucheza na timu za hapa, au kufananishwa tu na uchezaji wao.

Miaka ya 1980 na kuendelea, wachezaji wengi wa Tanzania walipewa majina ya wachezaji wa timu zingine za nje ya nchi, hasa wa Afrika Magharibi na zile za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Leo tunawataja wachezaji wa Kibongo waliopewa majina ya mastaa wa bara la Afrika wakati huo.

### JUMA PONDAMALI 'MENSAH'

Pondamali ni golikipa wa Pan African, Yanga na timu ya Taifa, Taifa Stars, kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1980 hadi mwishoni mwake. Ni mmoja kati ya makipa 10 bora wa Tanzania na timu ya taifa wa muda wote.

Anasifika si kwa kuwa kipa mzuri, lakini pia mbwembwe, utemi na aina fulani ya ukorofi akiwa langoni.

Miaka ya hivi karibuni aliwahi kuwa kocha wa makipa wa timu ya Yanga.

Mashabiki wakampachika jina la 'Mensah'. Huyu ni nani? Robert Mensah alikuwa ni golikipa wa timu ya taifa ya Ghana na Asante Kotoko ya nchini humo.

Ndiye aliyekaa langoni mwaka 1969 wakati Yanga ikicheza dhidi ya Asante Kotoko.

Mechi ya kwanza ya Klabu Bingwa Afrika hatua ya robo fainali, ikichezwa Oktoba 10, 1969 nchini Ghana, zikatoka sare ya bao 1-1, na mechi ya marudiano ilichezwa nchini Oktoba 30 mwaka huo, Yanga ikatolewa kwa penalti 4-3.

Katika mechi zote hizo, Mensah alikuwa shujaa na kuwa midomoni mwa mashabiki wa soka nchini.

Haikushangaza jina hilo wakampa Pondamali kutokana na kushabihiana kila kitu, ikiwemo mbwembwe, hadi wakati mwingine kudaka huku akiwa amevaa kofia.

### HASSAN ISIHAKA 'CHUKWU'

Hassan, alikuwa ni mmoja wa mabeki wa kati mahiri nchini wa timu ya taifa, Taifa Stars pamoja na Yanga mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Kutokana na uchezaji wake, mashabiki wakampachika jina la 'Chukwu.' Walimfananisha na beki wa kati wa timu ya taifa ya Nigeria, na Enugu Rangers ya huko Christian Chukwu.

Mashabiki wa soka Bongo walimuona laivu akiichezea timu yake hiyo dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Klabu Bingwa Afrika hatua ya robo fainali mwaka 1975, hasa Dar es Salaam katika mechi ya marudiano iliyopigwa Mei 25, 1975, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 na Yanga kutolewa hatua hiyo kwa bao la ugenini, baada ya mechi ya kwanza nchini Nigeria iliyochezwa Mei 11 mwaka huo kutoka suluhu.

### FRANK KASANGA 'BWALYA'

Alikuwa ni beki wa kati ya klabu ua Nyota Nyekundu, kabla ya kuhamia Simba katikati ya miaka ya 1980.

Frank Kasanga alikuwa mmoja wa mabeki mahiri, watata na wapambanaji kiasi cha mashabiki kumpachika jina la Bwalya.

Jina alilopewa ni la Harrison Bwalya, mmoja wa viungo wakabaji mahiri miaka ya 1980 wa timu ya taifa ya Zambia na timu mbalimbali za nchi hiyo na baadaye nje ya nchi.

Ukabaji wa beki huyo ulifananishwa na wa kiungo mkabaji huyo wa Zambia ambaye Wabongo walishuhudia kwenye michuano ya Kombe la Challenge lililochezwa nchini akiwa na timu yake ya taifa.

Bwalya alipoondoka hakuondoka na jina, lilibaki na wakampa Kasanga.

### ATHUMANI JUMA 'CHAMA'

Jina lake kamili aliitwa Athumani Juma. Lakini halikunoga, au kukamilika kama hukumalizia na Chama.

Alikuwa beki wa kati wa Yanga katikati ya miaka ya 1980 hadi mwishoni, akiwa na sifa zote anazotakiwa kuwa nazo beki. Mbishi, mpambanaji, na wakati mwingine katili kwa washambuliaji.

Kwa nini alipewa jina la Chama?

Lilikuwa ni jina la beki kitasa wa kati wa timu ya taifa ya Zambia kuanzia miaka ya 1967 hadi 1976, Dick Chama.

Alizichezea klabu za Mufulira Wanderers, Bancroft Blades, na Zambia Army kabla ya kutundika daluga mwaka 1976.

Beki hiyo alijipatia umaarufu mkubwa Ukanda wa Afrika Mashariki Kati na Kusini, na hapa Tanzania ilifika wakati beki yoyote akicheza vizuri tu wanampachika jina la Chama, kiasi kuwa na Chama wengi sana kwenye soka la mitaani hadi shuleni kwa wanafunzi.

Hata hivyo, Athumani Juma lilimkaa vema jina hilo alilopewa kiasi cha kuonekana kama jina lake kamili.



Athumani Juma 'Chama'



Robert Mensah



Juma Pondamali 'Mensah'

## HABARI KIMATAIFA

# Mapigano makali yaitikisa tena Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MILIPUKO ya mabomu na milio ya risasi imetikisa tena Ukanda wa Gaza na kuashiria vita iliyosimama kwa siku kadhaa kupisha ubadilishaji mateka kati ya Israel na wanamgambo wa Hamas imeanza tena.

Vyombo mbalimbali vya kimataifa, vimeripoti kwamba imesikika milipuko mikubwa na ufyatuaji risasi kaskazini mwa Ukanda wa Gaza.

Kulingana na mwandishi wa Al Jazeera, Tareq Abu Azzoum, matukio hayo yaliambatana na kuruka kwa ndege za kijeshi za Israel katika anga ya Ukanda wa Gaza.

Shirika la Habari la Ufaransa (AFP) lilinukuu watu walioshuhudia wakisema ndege za kijeshi zilizobeba mabomu yenye uzito mkubwa zilionekana zikishambulia eneo la kaskazini magharibi mwa Gaza

Hapo awali, Jeshi la Israel lilisema lilitungua roketi zilizorushwa karibu na mpaka wa Gaza.

Wakati hayo yakijiri, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani,Athony Blinken alitoa ujumbe mzito kwa Israel kuhusu kuanza kwa mashambulizi hayo.

Blinken alisema Benjamin Netanyahu ameweka wazi kuwa Israel inakusudia kurudi na operesheni zake za kijeshi, jambo ambalo linaweza kufanyika ndani ya siku chache.

Hata hivyo, Waziri huyo alisema oparesheni hiyo haiwezi kuwa ya kikatili kama ilivyokuwa nyuma na kuathiri maisha ya raia wa Kipalestina.

Mchana wa jana mashambulizi makubwa ya anga yalitawala mji wa Gaza na kushuhudia wingu likitanda juu angani.

Aidha, Hamas nao walijibu mapigo kwa kurusha makombora kutoka Gaza kuelekea Israel na kudunguliwa na mfumo wa Israel wa kujilinda dhidi ya makombora wa Iron Dome.

Hakuna dalili iliyoonyesha kwamba mapigano hayo ni ya kiwango cha chini kama ilivyoelezwa na Marekani, badala yake ukali wa mashambulizi yamekuwa kama ilivyokuwa awali.

Wakati huo huo, Jeshi la Israel liliangusha vipeperushi vya kuwataka wakazi wa mji wa Khan Younis kusini mwa Gaza kuondoka na kuelekea kusini zaidi kwa usalama wao.

Picha zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha moja ya kipeperushi hicho, ambacho kilisema mji huo wa Khan Younis ni eneo hatari la mapigano no na hivyo watu wa maeneo ya mashariki waondoke waelekee eneo lililopo karibu na Rafah katika mpaka na nchi ya Misri.

Vipeperushi kama hivyo pia vilikuwa vikisambazwa katika baadhi ya maeneo wakati vita hiyo ilipoanza, kama njia inayotumika na jeshi la Israel kupunguza madhara kwa raia wengi.

Muda mchache baada ya mapigano hayo kuanza tena, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alisema kitendo cha Hamas hatokubali kuwaachilia mateka zaidi, wamekiuka masharti ya makubaliano ya kusitisha mapigano. Ofisi ya Netanyahu ilitoa taarifa fupi ikieleza Hamas haikuwaachilia mateka wanawake wote kama ilivyokubaliwa, badala yake iliishambulia Israel kwa roketi asubuhi ya jana.

Hata hivyo taarifa hiyo iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, ilieleza Israel imeendelea kuwa na nia ya kufikia malengo yake ya kuwapata mateka, kuwaondoa Hamas na kuhakikisha Ukanda wa Gaza hautokuwa tishio kwa Waisrael.

**BBC**



Wakazi wa mji wa Gaza wakiondoka katika nyumba yao iliyoachwa kifusi baada ya kupigwa na bomu.**PICHA: REUTERS**

## Viongozi mkutano COP28 waanza kuhutubia

**DUBAI,** FALME ZA KIARABU

VIONGOZI mbalimbali wamewasili Dubai kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa kimataifa wa mazingira wa COP28, ambao unatarajiwa kuongeza shinikizo la kupunguza kiwango cha joto duniani.

Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) Sheikh Mohammed bin Zayed Al Nahyan aliwapokea viongozi hao kutoka mataifa mbalimbali ulimwenguni wakiwemo wakuu wa nchi tajiri akiwamo Mfalme Charles wa III wa Uingereza, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron na Waziri Mkuu wa India Narendra Modi.

Mkutano huo COP28 ulianza juzi Alhamisi kwa kukubaliana kuanzisha mfuko wa kukabiliana na hasara na uharibifu kwa nchi zilizoathirika na majanga ya asili.

Viongozi hao wameanza kuhutubia mkutano huo na siku mbili zijazo Mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed Bin Salman ambaye nchi yake ni mzalishaji mkuu wa mafuta, na Waziri Mkuu wa India Narendra Modi, ambaye mji yake mikubwa inachangia uchafuzi wa hali ya hewa watapewa nafasi ya kuongea katika mkutano huo.

Hata hivyo viongozi wa mataifa mawili makubwa ambayo ni wazalishaji wakubwa wa hewa chafu ya kaboni ambayo inachangia kwa zaidi ya asilimia 44, Rais Marekani Joe Biden wa China, Xi Jinping hawatokuwepo.

Mfalme Charles wa 111 wa Uingereza alihutubia hadhira hiyo akisema kwamba mkutano wa mwaka huu unapaswa kuwa na dhamira ya kweli ya kuleta mageuzi.

"Ninasali kwa moyo wangu wote kwamba COP28 utakuwa mkutano mwingine muhimu kuelekea hatua thabiti za mageuzi katika wakati ambao tayari, kama wanasayansi walivyokwisha kuonya kwa muda mrefu, tunashuhudia kufikia hatua za kutisha," alisema Mfalme Charles.

## Milio ya risasi yasikika Guinea Bissau

**BISSAU,** GUINEA-BISSAU

MAJIBIZANO ya risasi yameripotiwa kutokea katika mji mkuu wa Guinea-Bissau jana asubuhi baada ya wanajeshi wa kikosi maalum kwenda kuwaondoa viongozi wa serikali waliowekwa kizuizini.

Wanajeshi waliwachukua maofisa hao akiwemo Waziri wa Fedha Souleiman Seidi, na katibu wa hazina kuu ya serikali, Antonio Monteiro na kuwapeleka katika kambi ya kijeshi iliyoko kusini mwa mji mkuu.

Kikosi hicho maalum kiliingilia kati baada ya mazungumzo ya kuwaachia huru kukwama na kusababisha kuibuka kwa mapigano ya pande mbili za wanajeshi.

Hata hivyo, hali ya utulivu imerudi tena baada ya kutoka tukio hilo.

Shirika la habari la Ufaransa (AFP) lilieleza kiongozi wa kundi la wanajeshi waliokuwa wakijaribu kuwaachilia kinguvu viongozi hao wanashikiliwa na jeshi na hali imedhibitiwa.

Waziri huyo na katibu wa hazina walikuwa kizuizini wakati wakifanyiwa uchunguzi wa madai ya kutolewa kwa dola milioni 10 ya fedha za serikali kwa njia isiyo ya kawaida. Viongozi hao walihojiwa Alhamisi alasiri na uchunguzi ulianzishwa dhidi yao kubaini malipo yenye utata yaliyofanyika kwa kampuni 11. Katika kikao cha bunge kilichofanyika Jumatatu ya wiki hii, kiongozi wa chama kikuu cha upinzani nchini humo alidai kuwa wamiliki wa kampuni hizo zinazodaiwa kupewa malipo walikuwa karibu na viongozi wa serikali ya muungano unaotawala nchi hiyo.

**BBC**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**NASHON WILLIAM UTENGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0449/0177** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **J.J. MUNGAI SEKONDARI** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/442649/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**IDD MUSA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.333/195** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWANZA SEKONDARI mwaka 2003. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **OB/RB/6948/2014.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MALIAKI JOEL LUKUMAY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 563 AZA.** Chassis namba **LMHPCJL7480901152.** Engine namba **157FM180605848.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8161/2023.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**

**MISC. CIVIL APPLICATION NO. 72 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SHIRAZ BADRUDIN SHARIFF**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR CITATION TO ACCEPT OR RENOUNCE EXECUTORSHIP**
**BY**
**OMAR SHARIFF.............APPLICANT**

**CITATION TO ACCEPT OR RENOUNCE EXECUTORSHIP**
**(Rule 27(2))**
**TO: FATEH SUNDERJI And AZMAIRNIN JADAVJL.**

**WHEREAS** it appears by the affidavit of OMAR SHARIFF, affirmed on 26th day of **OCTOBER, 2023 that SHIRAZ BADRUDIN SHARIFF** of Dar es salaam died on the 22nd day of January, 2023 at Saifee Hospital at Kinondoni Dar es salaam, having made and duly executed his last Will and testament dated the day of 21st January, 2021 and thereof appointed you, the said **FATEH SUNDERJI and AZMAIRNIN JADAVJI** as excutors. Now this is to command you, the said **FATEH SUNDERJI** and **AZMAIRNIN JADAVJL**, that within 21 days after service hereof on you, inclusive of the day of such service, you do cause an appearance to be entered by you in the High Court Registry at Temeke and accept or refuse probate of the said Will. And take notice that, in default of you so appearing you shall be deemed to have renounced you right and title to the execution of the said Will.

**Dated at Dar es salaam this 07th day of November, 2023.**

DEPUTY REGISTRAR

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26467 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late MALONGO IDEBE MALONGO of MIYUJI KIBAONI Area within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MUSSA MALONGO IDEBE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 4 Day of 1, 2024
Dated at Dodoma this 27th day of NOVEMBER 2023

.......................................................
PETITIONER
Presented for filing this 30th day of NOVEMBER 2023

.......................................
RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODSON ELIMBINZI MAUKI,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo Chenye no **IRDP/BDF/13/588** kilicholewa na chuo cha **INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING** Mwaka 2016. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/10574/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JORDAN NICKODEMAS RUTASHOBYA,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Nne chenye Index no **S0578/0185** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya secondari Taqwa Mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/5640/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHRISTOPHER BONI KISETU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 775 AEV – DEFENDER 10.** Chassis namba **SALLADHAF7MA948451** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8161/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHATO**

**Kituo cha CHATO MJINI Mkoa GEITA**

**Shauri la Madai/ Ndoa Na.55 Mwaka 2021**

**Jina la Mdai DAUD EMMANUEL MANYAMA**

**Jina la Mdaiwa PROCHES PROSPER TEGAMAISHO**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: PROCHES PROSPER TEGAMAISHO**

**KWAMBA:** Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa Hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii Tarehe 4/12/2023 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29/11/2023

.......................
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**CHATO MJINI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya BUGANDO Wilaya ya GEITA Mkoa ............................... GEITA**

**Shauri la MADAI Na 96/2023**

**Jina la Mdai.........................................JONASI SIMON**

**Jina la Mdaiwa.......................................MOSHI ELIAS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:MOSHI ELIAS**
**WA NKOME**

**AMRI: -** Unaamriwa na Jamuhuri uhudhurie Mahakamani hapa siku ya Jumanne tarehe 4/12/2023 saa 2:00 Asubuhi ili ujibu madai ya Fedha Tsh. 3,020,000/- za mdai. Usipohudhuria kesi itasikilizwa bila wewe kuwepo
Unaonywa usikose kuhudhuria.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 20 Mwezi 11 Mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

# Mama mwenye nyumba-4

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Umasikini wako, ungejenga ya kwako!" Mwantumu akadakia.

"Wewe ya kwako? Si umerithi tu ya mama yako. We mwenyewe una ubavu huo? Hali yako ya mkunga ukijikuna unatoka unga, una ubavu huo?"

"Nyinyi mnamuona huyu ananitukana eee. Nakwambia leo natoa makochi yako mabovu nje."

"Thubutu, bila kuniridhishia kodi yangu? Nipe kodi yangu kwanza uone kama nitang'ang'ania kijumba chako kibovu hiki."

"Mbona unakaa?"

"Mimi nilijua? Si nililetwa na madalali tu. Nasubiri tu kodi yangu ikiisha kama utaniona."

Hali ilizidi kuwa mbaya, kiasi kwamba iliokana kama wanawindana. Devota na mama wa jirani, walimvuta Tabia na kumuingiza chumbani kwake, wakafunga mlango kwa nje.

"Utawaonea wapangaji hao hao wanaokutetemekea siyo mimi!"

"Kelele, baamedi mkubwa we." Mama mwenye nyumba naye akajibu.

*****************************************

"Mama Mwadawa hebu nisaidie mwenzangu."

"Nini tena mama Abdul?"

"Unakumbuka wiki iliyopita tulivyokwenda kwenye kicheni pati ya binti wa mama Maua?"

"Ndiyo nakumbuka kule Koma Koma."

"Ndiyo. Basi mwenzangu, mume wangu alikuwa anapiga simu kila baada ya dakika moja, nilipokea hatuelewani makelele ya mle ndani na kutoka siwezi kutoka kwenda mbali. nikaamua tu nizime na sikupokea tena, mama wee, niliporudi, hukuwepo lakini malaika wako walikuwepo, yule baba alinitukana. Hakunibakisha kitu, kanitukania mpaka wazazi wangu, eti hawakunifunda vizuri. Hivi ninavyokwambia hadi leo tumeniniana."

Mama Abdul ana undugu na Mwantumu. Wiki iliyopita walipokwenda kwenye kicheni pati na akakorofishana na mumewe, mtu aliyeona sahihi wa kwenda kumwambia shida yake na wa kumsaidia ni Mwantumu tu.

Hakutaka njia ya kupatana. Alichotaka ni mtu ambaye anaweza kumpa makavu laivu mumewe kwani aliona alichofanya sicho.




Alikuwa ametoka Temeke kwenda Magomeni Mapipa kwa ajili hiyo tu.

"Hivi alipoondoka tu kwenda kazini nimetoroka kuja huku. Nataka umnyambue maana kazoea, ndiyo maana nimekuja kwako, maana kazi hiyo unaweza shangazi."

"Hivi mumeo huyo ana wazimu? Hebu nijazie vocha nimpigie, yaani muda wote yeye anawaza kuwa wanawake wanakwenda kufanya uhuni kwenye sherehe." Kwa Mwantumu upele ulikuwa umepata mkunaji.

"Sasa unasikia shangazi, usiseme kama mimi nimekuja huku, wewe sema tu tuliona siku ile umempigia simu mkewe unamsumbuasumbua." Mama Abdul akatahadharisha.

"Wala usipate shida, zima kabisa hiyo simu yako, asije akakupigia halafu akajua upo hapa, bora uizime kama akiwasha baadaye umwambie ulikuwa unachaji, upo hapo?"

Mama Abdul alimpa mama Amina buku tano ya vocha. Lakini hakununua. Aliiweka kibindoni. Tayari alikuwa na muda wake maongezi.

Akatafuta namba za huyu bwana. Ni mume wa mama Abdul. Akabonyeza, ikaanza kuita, akamkonyeza mwenyewe.

"Habari yako Baba Abdul?" Akasalimu na salamu ikaitikiwa.

"Unasikia Baba Abdul mimi tabia yako sijaoipenda kabisa uliyoifanya wiki iliyopita!"

"Ipi hiyo?" Swali liliulizwa upande wa pili.

"Wanawake tupo kwenye kicheni pati, wewe tena dume zima unafanya kazi ya kumpigia simu mkeo kama askari polisi anatafuta mhalifu..."

"Siyo hivyo, mimi nilitaka kujua tu kama amefika!"

"Siyo kweli bwana, wewe si ulimpigia mara ya kwanza akapokea. Ukasikia makelele za muziki? Sasa ulijua yupo disco na mabwana eee!"

"Hapana mama Mwadawa..."

"Si tulikuja kwako na sare, tukakuomba kama mumewe, na kadi tukakuonyesha, ukakubali, sasa kisa cha kumpigia mkeo simu, na kesho yake aliporudi ukamtukana hadi leo hii ugomvi haujaisha ni nini we baba? Au hutaki mkeo kwenda kwenye shughuli za ndugu au shoga zake? Ukiendelea na tabia hii tutamtenga mkeo." Mwantumu alizidi kukichafua.

Mama Abdul alikuwa akimtazama, akitabasamu na kumkonyeza kuwa aongeze mashambulizi.

"Unasikia, wanawake wote waliokwenda kwenye kicheni pati siyo kama hawana waume. Wana waume zao na hata kama hawajaolewa lakini wana wanaume wanaoishi nao pika na kupakua. Lakini wenzako wana akili. Usidhani watu wanakwenda kwenye shughuli wanafuata mabwana, zile ni shughuli za kijamii ambazo mwanamke yoyote atapitia, sasa kama hujaenda kwa wenzako likikupata na wewe unakuwa mgeni wa nani?"

"Basi mama Mwadawa samahani!" Jamaa akaomba msamaha.

"Eee, ujirekebishe bwana, nasikia si mara moja wala mbili, una wivu usio na maana, kwani huyu mkeo umemuoa akiwa mdogo? Si mtu mzima, sasa..."

"Sasa kama ni kweli umeomba kwa dhati huo msamaha, nataka leo mmalizane na mkeo. Muongee na sitaki kusikia tena unamtukana."

"Sawa nitatekeleza hilo." Baba Abdul akajibu na mama Mwadawa akakata simu.

"Nimemchamba, harudii tena!"

Mama Abdul akaangua kicheko. "Ndiyo dawa yake, mwanaume ana wivu kama kicheche."

"We mama Mwadawa, mbona makelele kama umepokea mshahara mpya?" Sauti ya kike ilisikika na dada mmoja jirani aliyekuwa anapita kwenda nyumba ya pili kuchota maji.

"Kuna mtu nilikuwa nampa vipande vyake kwanza, si unanijua zangu," akajitapa mama mwenye nyumba huyo.

Siku hiyo wapangaji wake walipumzika, maana alikuwa ameshapata mtu wa kusemezana naye ameridhika.

Mama Abdul alipokuwa akiaga tu, Mwantumu akapata mgeni mwingine. Ni Bishada.

Haraka haraka, akajua nini amefuata. Umbea. Akakumbuka siku ile alipokutana naye njiani alimuahidi kumpa maneno.

"Kwanza nilitaka kukufuata nikupe taarifa ya shughuli shoga yangu, miezi miwili ijayo, dada yangu Mkuranga anaozesha, halafu nikupe umbeya.

Huu ubea wako mwenyewe. Wanavyokuengelea. Yaani shoga yangu ukiwa unaongea na watu, ukiwapa kisogo tu, wanakung'ong'a. Wanakuongelea vibaya dada yangu, yaani wewe hapo huna nguo."

Akakumbuka kuwa hakukuwa na umbea wowote, ila ilikuwa ni kupoza joto la kudaiwa taiti, gauni na blauzi.

Hata hivyo hakijaaribika kitu, akajiandaa kutunga uongo. Kumsingizia mtu. Akajiuliza amsingie nani?

"Karibu shoga yangu Bishada" Akamkaribisha kwenye mkeka.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

**Huu ubea wako mwenyewe. Wanavyokuengelea. Yaani shoga yangu ukiwa unaongea na watu, ukiwapa kisogo tu, wanakung'ong'a. Wanakuongelea vibaya dada yangu, yaani wewe hapo huna nguo.**

## HABARI MICHEZO

# KIDUKU KUMKABILI SEBIYALA USIKU WA MABINGWA 2023

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Mtanzania Twaha Kiduku anatarajia kupigana na Mohammed Sebiyala kutoka Uganda katika pambano la kimataifa la Usiku wa Mabingwa lililopangwa kufanyika Desemba 26, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

**Akizungumza jijini jana, Mratibu wa matukio wa PEAKTIME, Bakari Khatibu, alisema lengo kuandaa Usiku wa Mabingwa ni kusherehekea na kutambua mchango kwa mabondia waliofanya kazi na kampuni yao pamoja na mapromota wengine kwa mafanikio.**

Khatibu alisema maandalizi kuelekea vizuri msimu wa tano na tayari mabondia wote watakaoshiriki wamesaini mikataba ya kuthibitisha kupanda ulingoni.

Alisema huu ni msimu wa tano na wanatarajia kila bondia ataonyesha ushindani ili kuwapa burudani mashabiki na wadau wa mchezo wa ngumi nchini.

"Kuelekea pambano hilo lililobeba kauli mbiu 'Wanyama Wamerudi Nyumbani' kila kitu kinakwenda vizuri, tayari mabondia watakaopanda ulingoni siku hiyo wamesaini mikataba yao na tunatarajia kufanya zoezi la kupima afya ifikapo Desemba 12, mwaka huu," alisema Khatibu.

Naye Mjumbe wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Abdallah Juma, alisema taasisi hiyo imebariki pambano hilo na wanawataka mabondia waendelee kujiandaa vyema.

Juma alisema Peaktime imekuwa ikifanya kazi nzuri ya kuibua vipaji vipya ambavyo vitasaidia kuendeleza mchezo huo.

Kiduku alisema amejipanga kurejea kivingine baada ya kupoteza pambano lake lililopita.


Alisema atahakikisha anafanya vizuri katika pambano lake ingawa alikiri atakutana na mpinzani mwenye uwezo na uzoefu.

"Baada ya kupoteza pambano lililopita sasa ninarudi kwa kasi nyingine na kwa hamu, najua Waganda wana balaa zito, lakini mpinzani wangu ajue amekanyaga nyoka mkia, tukutane Desemba 26," alisema Kiduku.

Kwa upande wake, Francis Miyeyusho 'Chichi Mawe', alisema amejianda vizuri kuondoka na ushindi dhidi ya mpinzani ambaye atakutana naye.

"Ninaahidi kuwapa furaha Watanzania, nawaomba wajitokeze kwa wingi katika usiku huu maalumu ambao utakuwa wa kihistoria, mimi binafsi nimejipanya vya kutosha kwa mpambano huo," Miyeyusho alisema.





Msemaji wa Kampeni ya Magifti Dabodabo, Haji Manara (katikati) akimtangaza mmoja wa washindi wa safari ya Dubai, Victor Munisi (kulia) wa Dar es Salaam, kushoto ni rafiki wa karibu wa mshindi huyo, Jonhson Julius ambaye atakwenda naye Dubai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Washindi Tigo Magifti wapatikana*

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wa kwanza wa kampeni ya wateja ya Magifti Dabodabo inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo wametangazwa rasmi jana na kukabidhiwa zawadi zao.

Akizungumza wakati akiwatangaza washindi hao jijini jana, Mkuu wa Wateja Maalum wa Tigopesa kutoka Tigo, Mary Rutta, alisema washindi hao ni wa kwanza baada ya kampeni hiyo kuzinduliwa wiki iliyopita.

Alisema washindi waliopatikana ni wale wa fedha, vocha ya safari ya kwenda Dubai na Zanzibar pamoja na washindi wa vifaa vya umeme vya majumbani.

"Kama tulivyosema wakati wa uzinduzi wa shindano hili, kila mshindi atakayeshinda zawadi yoyote atachagua mtu mpendwa wake mmoja ambaye naye atapewa zawadi sawa na aliyoshinda mshindi, hii ndio sababu tukaiita kampeni hii kuwa ni 'magifti dabo dabo'," alisema Mary.

Aliwataja washindi walioshinda safari ya Dubai ni Meshack Justine wa Dar es salaam ambaye amechagua kwenda safari hiyo na mke wake huku mshindi mwingine wa zawadi hiyo, Victor Munisi wa jijini amesema ataenda rafiki yake wa karibu, Johnson Julius.

"Mshindi wa safari ya Zanzibar ni Aisha Kajilu, huyu amechagua kwenda na mume wake, safari za washindi hawa zitakuwa Desemba 11, mwaka huu. Tunasisitiza watumiaji wa tigo kuendelea kufanya miamala ya fedha na kununua vifurushi mbalimbali ili kushinda," alisema Mary.

Alimtaja Omega Boniface yeye ameshinda zawadi ya seti ya vifaa vya umeme vya ndani ambavyo ni friji, microwave, televisheni na redio ya kisasa.

# New City yaamka Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya New City FC imeendelea kupata matokeo mazuri baada kuwafunga Wanajeshi wa Kipanga mabao 2-1 katika mechi ya mzunguko wa 13 ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau B juzi jioni.

Kwa matokeo hayo New City imefikisha pointi 13 lakini bado iko katika mstari wa hatari wa kushuka daraja, wako katika nafasi ya 14 kati ya timu 16 zinazoshiriki ligi hiyo.

Timu nne zitakazoshika mkia katika msimamo wa ligi hiyo ambayo bingwa wake atapata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, zitashuka daraja.

New City FC imeshinda mechi tatu kati ya ka michezo 13 waliyocheza, wametoka sare michezo minne na michezo sita wamepoteza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa New City, Razak Salum Rajab, alisema licha ya kupata ushindi katika mechi mbili mfululizo lakini bado timu hiyo iko katika hali mbaya.

Kocha huyo alisema wanahitaji kupata ushindi katika michezo mingine inayofuata ili kujinusuru na janga la kushuka daraja lakini pia wakiwaita mashabiki wao kujitokeza kuwasapoti.

Alisema Ligi Kuu Zanzibar inazidi kuwa ngumu kwa sababu timu zinaonyesha ushindani na zinatofautiana pointi chache kutokana na matokeo ya sare wanayopata.

"Kwa sasa kikosi changu kimeimarika na wachezaji wanajituma, hali hii inanipa matumaini, tunaelekea pazuri, endapo tutashinda michezo ijayo, tutajiweka sehemu salama.

Wachezaji hivi sasa wameshazoea mikimiki ya Ligi Kuu, wameimarika na wanacheza vizuri ikilinganishwa na hapo awali wakati tunaanza msimu, hali hii inaweza kutusaidia kufanya vyema hapo baadaye,"aliongeza kocha huyo.

New City itashuka tena uwanjani kusaka pointi muhimu Desemba 9, mwaka huu kuvaana na KVZ FC.

**Kwa sasa kikosi changu kimeimarika na wachezaji wanajituma, hali hii inanipa matumaini, tunaelekea pazuri, endapo tutashinda michezo ijayo, tutajiweka sehemu salama.**

## ZISIKUPITE

### WILLIAN AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Manchester United imeungana na Manchester City, Chelsea, Bayern Munich, Borussia Dortmund na Real Madrid katika mbio za kumsaka winga wa Palmeiras Mbrazil Estevao Willian mwenye umri wa miaka 16. ***(Teamtalk).***

### JOTA KUMFUATA ANGE

WINGA wa Al-Ittihad, Jota mwenye umri wa miaka 24 anataka kuungana na kocha wake wa zamani wa Celtic, Ange Postecoglou, katika klabu ya Tottenham Hotspur. ***(Sun)***

### GUIRASSY AGEUKA LULU

KLABU ya Manchester United pia imeungana na Newcastle, Roma na AC Milan katika kinyang'anyiro cha kumnunua mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27. ***(Foot Mercato)***

### UNITED YATAKA YOSSO

MWEKEZAJI wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, anataka timu yake isajili vipaji vya nyumbani katika kipindi cha usajili wa majira ya joto. ***(Mail)***

### TOMIYASU, ARSENAL SAFI

ARSENAL iajadiliana na mlinzi wa Timu ya Taifa ya Japan, Takehiro Tomiyasu, kuhusu mkataba mpya huku baada ya ule wa awali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ukitarajiwa kukamilika 2025. ***(Athletic)***

### DRAGUSI ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inajadiliana kuhusu usajili wa beki wa Timu ya Taifa ya Romania na Genoa, Radu Dragusin, mwenye umri wa miaka 21. ***(Prosport)***

### ILING-JUNIOR SOKONI

BEI ya winga wa Juventus, Samuel Iling-Junior, mwenye umri wa miaka 20 sasa imetajwa kuwa ni euro milioni 18 kutoka euro milioni 20, na Tottenham wanavutiwa na mchezaji huyo. ***(Calciomercato)***

### GUEHI: NITABAKI CRYSTAL

MARC Guehi anataka kusalia Crystal Palace hadi usajili wa majira ya joto ili kuongeza nafasi yake ya kujiunga na kikosi cha England kwa ajili ya Euro 2024. Beki huyo mwenye umri wa miaka 23 anawindwa na Manchester United na Newcastle United. ***(90 min)***

### NYOTA AITAKA MADRID

MCHEZAJI wa Napoli, Khvicha Kvaratskhelia, mwenye umri wa miaka 22 ambaye anasakwa na Chelsea huenda akavutiwa zaidi kujiunga na Real Madrid, kwa mujibu wa babake yake. ***(Geo Team, via Express)***

### PAQUETA MAMBO MAGUMU

KLABU ya Manchester City iko tayari kuachana na mpango wa kumnunua kiungo wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta, mwenye umri wa miaka 26, ikiwa suluhu kuhusu uchunguzi wa kamari dhidi ya mchezaji huyo hautakuwa imepatikana. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CARRAGHER AINYIMA ARSENAL TAJI LA EPL

**Mchambuzi huyo asema bado timu hiyo haina kiwango bora cha...**

**LONDON,** England

MCHAMBUZI wa soka wa England kupitia kituo cha televisheni cha Sky Sports na mchezaji wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher, amesemna Arsenal haiwezi kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu wa 2023/24.

**Garragher amedai anafuatilia mechi zao zote na anaamini kuna uwezekano mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England zikakwama kwao kutokana na kiwango chao msimu huu.**

Hata hivyo, Arsenal imependa nafasi ya kwanza katika msimamo wa ligi hiyo baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Brentford wikiendi iliyopita ikiwazidi Manchester City kwa tofauti ya pointi moja tu.

Huo unakuwa ushindi wa tano kwa Arsenal baada ya mapumziko ya kimataifa huku Kai Havertz akiibuka shujaa kutokana na kufunga bao la ushindi dakika ya 89 akitokea benchi.


Mkongwe huyo alidai Arsenal bado inakabiliwa na changamoto kwenye safu ya ushambuliaji hivyo kocha, Mikel Arteta ana kazi ya kufanya kama amepania kubeba ubingwa, kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2003-2004.

"Bado tumebaki na nusu ya msimu, kama Arsenal itaendelea kucheza hivi na kiwango kidogo sidhani kama ina nafasi ya kubeba ubingwa msimu huu, mechi za ligi zina upinzani mkali, tuliona makosa ya kipa, Aaron Ramsdale, dhidi ya Brentford wikiendi iliyopita, angeigharimu timu na tuliona Arsenal ilivyopambana kupata ushindi kipindi cha pili."

Carragher alisisitiza Arsenal imekosa muunganiko na nguvu ambayo iliwafanya kuwa hatari msimu uliopita licha ya kukosa ubingwa zikiwa zimebaki mechi tano msimu ligi kumalizika.

"Nadhani tunaiongelea Arsenal tofauti msimu huu, hata takwimu zao unaona msimu huu, lakini kila mtu ataona kwa macho yake, Arsenal sio kama ya msimu uliopita, haina nguvu, hata nafasi wanazotengeneza ni chache sana. Hata safu yao ya ushambuliaji imekuwa ya kawaida sana."

# TEN HAG: ONANA BADO NAMBA 1



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, ataendelea kumuunga mkono, André Onana, kama mlinda mlango wake chaguo la kwanza na bado anaamini ulikuwa uamuzi sahihi kumleta baada ya kuondoka kwa David De Gea msimu uliopita wa joto, kwa mujibu wa ESPN.

Onana alifanya makosa mawili makubwa katika sare ya mabao 3-3 dhidi ya Galatasaray, mechi iliochezwa kwenye Uwanja wa Rams Park jijini, Istanbul na United ikatolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Si mara ya kwanza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kufanya dosari wakati wa mwanzo mgumu wa msimu wake wa kwanza Old Trafford, lakini kwa mujibu wa ESPN, Ten Hag anaamini usajili wa pauni milioni 43 kutoka Inter Milan umegeuza mambo.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN, Ten Hag anaimani na Onana kwa safari ya Ligi Kuu England watakapoikabili Newcastle United leo, isipokuwa kama mlinda mlango huyo ataweka wazi anataka aondolewe kwenye kikosi hicho.

Onana aliletwa kuchukua nafasi ya De Gea, ambaye alitumia zaidi ya mwongo mmoja kama namba moja pale wa United.

Makosa ya Onana yamesababisha baadhi ya mashabiki kumtaka De Gea arejee, lakini Ten Hag anaamini kuna faida nyingi za kumsajili kipa huyo wa zamani wa Ajax kwa sababu staili yake inaendana zaidi na Mholanzi huyo anavyotaka timu icheze.

Ten Hag alifurahishwa na pasi ya Onana aliyompa Alejandro Garnacho kuiwezesha United kuwa mbele kwa 1-0.

# Fati kukaa nje muda mrefu

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Brighton & Hove Albion, Roberto De Zerbi, amekiri anatarajia kumkosa mchezaji wa Barcelona, Ansu Fati, ambaye anacheza kwa mkopo wa "muda mrefu" baada ya kuumia hivi karibuni.

Fati, ambaye ana umri wa miaka 21, alijiunga na Brighton kwa mkopo wakati wa majira ya joto kujaribu kurudisha kasi yake ambayo imekuwa ikikumbwa na majeraha makubwa tangu alipoumia goti Novemba, mwaka 2020 lilimgharimu karibu mwaka wa maisha yake ya ujana.

Akikabidhiwa mwanzo wake wa pili wa msimu wa Ligi Kuu mwishoni mwa wiki, Fati alicheza dakika 21 tu dhidi ya Nottingham Forest kabla ya kuchechemea hadi kwenye benchi, na ripoti zinaonyesha anakabiliwa na miezi mitatu nje ya uwanja kwa shida ya misuli.

"Ansu na (Tariq) Lamptey wote wamejeruhiwa," alisema bosi wa Brighton, De Zerbi katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Tumewapoteza kwa muda mrefu nadhani."

Fati alifanikiwa kufunga mabao manne na kusaidia katika mechi 14 alizochezea Brighton na anaweza kukaa nje ya uwanja hadi Machi, mwakani.

Mapumziko kama haya kwa bahati mbaya sio kitu kipya kwa Fati. Baada ya miezi 11 nje ya uwanja kutokana na jeraha la goti, mfululizo wa matatizo ya misuli ya paja yalimfanya kuwa nje kati ya Novemba, 2021 na Aprili, 2022, ambapo alijitahidi kuonyesha kiwango chake bora zaidi kwa Barcelona.

Uamuzi huo ulifanywa wa kumtoa kwa mkopo Fati msimu huu wa joto na mchezaji huyo na kutua Brighton, ambapo amekuwa akitumiwa sana na De Zerbi.





# *Salah amtamani na De Bruyne*

**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool ma Misri, Mohamed Salah amebainisha mbali na Cristiano Ronaldo pamoja na Lionel Messi, mchezaji ambaye anatamani acheze naye timu moja ni, Kevin De Bruyne wa Manchester City.

Wawili hao ilibaki kidogo wacheze pamoja ndani ya Chelsea, lakini haikuwa hivyo baada ya kupishana klabuni na kila mmoja akikaa kwa miaka miwili.

Alianza De Bruyne kuwa mchezaji wa Chelsea, alikaa kuanzia 2012 hadi 2014, halafu Salah akatua hapo mwaka 2014 na kuondoka ilipofika mwaka, 2016.

"Katika maisha yangu ya soka, ningependa kucheza sambamba na Ronaldo na Messi, lakini mbali na hao, mchezaji ambaye ningetamani kuwa naye timu moja ni Kevin De Bruyne," alisema Salah akinukuliwa na ESPN.

Katika hatua nyingine, Salah amefichua ndani ya Ligi Kuu England, beki mgumu zaidi ambaye amewahi kukutana naye ni Cesar Azpilicueta aliyekuwa akitumikia Chelsea kuanzia 2012 hadi 2023, kabla ya kujiunga na Atletico Madrid ya Hispania.

Hata hivyo Salah kwa sasa ni mmoja wa wachezaji wa Ulaya wanaotakiwa na timu za Saudi Arabia.

## HABARI MICHEZO

# Kitambi aitaka nne bora Ligi Kuu Bara

Na Shufaa Lyimo

KATIKA kuhakikisha inazibakisha pointi tatu nyumbani, Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, amewapa mazoezi maalumu mastraika wake ili kuwaongezea mbinu za kufunga mabao kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Namungo itawakaribisha Dodoma Jiji katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Kitambi alisema lengo la kuimarisha safu hiyo ni kuhitaji kupata mabao mengi yatakayowasaidia kupanda katika msimamo wa ligi hiyo.

"Nitahakikisha ninaimarisha timu yangu ili msimu huu tushike nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tutaendelea kujiimarisha zaidi," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wako katika hali nzuri na kila mmoja ana morali ya juu ya kupambana na kusaka matokeo chanya.

"Nimewakumbusha kuingia uwanjani kwa tahadhari kwa sababu msimu huu hakuna timu ya kubeza, kila upande umejipanga kupambana kusaka pointi iwe nyumbani au ugenini," Kitambi alisema.

Aliongeza atafanya kila linalowezekana kuhakikisha timu hiyo inamaliza msimu kwenye nafasi za juu na kamwe isiwe katika kundi linalotaka kujinusuru na kushuka daraja.



# DEWJI AONYA WACHEZAJI 'WAVIVU, MIZIGO' SIMBA

Na Adam Fungamwango

KIONGOZI na mfadhili wa zamani wa Simba, Azim Dewji, amewaonya wachezaji ambao hawana nidhamu katika timu hiyo waanze kuhesabu siku baada ya ujio wa Kocha Mkuu mpya, Abdelhak Benchikha, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jijini, Dar es Salaam, Dewji, mwanachama mkongwe wa timu hiyo, aliyeiongoza kucheza fainali ya Kombe la CAF (sasa Kombe la Shirikisho Afrika), mwaka 1994 akiwa kama mfadhili mkuu, pia amewapongeza viongozi wa timu hiyo kwa kumnasa kocha huyo mwenye hadhi kubwa.

"Nawapongeza viongozi kwa kumpata kocha mwenye hadhi wa klabu ya Simba, amefundisha klabu nyingi kubwa na amepata mafanikio makubwa na kwa sura tu anaonekana mkali, nahisi hiki ndicho kinachotakiwa kwenye klabu kubwa kama hii, na kuwaongoza wachezaji wenye kaliba kama ya Simba.

Nadhani sasa timu inaweza kabisa kupata matokeo mazuri, nawasihi wachezaji kocha amepatikana, wampe ushirikiano," Dewji alisema.

**Aliwatolea uvivu wachezaji waliojiona mastaa sasa ni wakati wao kubadilika na kumpa ushirikiano kocha, vinginevyo wajiandae kuondoka, kabla ya kusajiliwa nyota wengine.**

"Kwa wachezaji, nataka niwaleze ambao hawataki kutoa ushirikiano na hawataki kucheza mpira waondoke na viongozi wasiwalee, bora tuwe na wachezaji wachache wanaojituma, wenye nidhamu, hata kama si wazuri zaidi ya wale ambao wasio na nidhamu, bora tubaki nao hao na najua baadaye tutapata wachezaji wazuri," aliongeza.

Simba imemnasa kocha huyo wa zamani wa USM Alger ya Algeria baada ya kuachana na Mbrazil Roberto Oliveira na hiyo ilikuja siku chache baada ya kupokea kipigo cha fedheha cha mabao 5-1 dhidi ya Yanga, mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.




Wachezaji wa Simba wakiwasili Botswana kwa ajili ya mechi ya Kundi B ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji wao, Jwaneng Galaxy itakayochezwa leo nchini humo. **PICHA: SIMBA SC**

# *Simba, Yanga fanyeni kweli*

INATOKA UKURASA 24

rika ya Kundi B ikiwa kwa mara ya kwanza chini ya kocha wake mpya, raia wa Algeria, Abdelhak Benchikha.

Akizungumza na gazeti hili, Benchikha alisema pamoja na kusaka ushindi, lakini itakuwa ni fursa ya kuangalia kwa ukaribu zaidi timu yake na wachezaji.

Benchikha alisema anatarajia kuona soka la kiwango cha juu kutoka kwa wachezaji wake ambao kila mmoja yuko tayari kusaka ushindi na kurejea kwenye furaha iliyopotea.

"Nilikuwa naifuatilia, na hata tulipokuwa katika mazungumzo nilianza kuzifutilia baadhi ya mechi za timu hii na wachezaji wake, nimeona, ila katika mechi hii nitaona mengi zaidi ambayo yatakuwa ndiyo ufunguo wa Simba ya baadaye kuelekea kwenye mafanikio makubwa tunayotarajia kuyapata huko mbele," alisema Benchikha.

Hii si mara ya kwanza kwa Simba kucheza Botswana na kupata ushindi, katika mechi ya raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyofanyika Oktoba 17, mwaka 2021 Mnyana aliifunga timu hiyo mabao 2-0, Thadeo Lwanga na John Bocco, wakitikisa vyavu.

Hata hivyo, Simba ilitolewa katika michuano hiyo kwa kufungwa mabao 3-1 katika mechi ya marudiano, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa iliifunga Jwaneng Galaxy ugenini.

# Shime: Bahati imetubeba Twiga

INATOKA UKURASA 24

tungepata nafasi mbili au tatu na kufunga mabao zaidi. Tumefanya makosa mengi ambayo yangeruhusu wapinzani wetu wakipata bao.

Mwisho wa siku tumekuwa na bahati. Tumeona makosa mengi, tutakuwa na utulivu mzuri wa kufanyia kazi mapungufu yetu kuelekea mechi ya marudiano," alisema Shime.

Aliongeza Tanzania tayari ina mtaji mzuri wa mabao 3-0 na ili waondolewe, Togo itawalazimu kuwafunga magoli kuanzia 4-0 jambo ambalo litakuwa gumu kutokea licha ya kumalizia kibarua hicho ugenini.

"Nitaenda kufanya kazi makosa yote yaliyojitokeza katika mchezo huu na kuweka sawa mipango yetu kwa ajili ya mchezo wa marudiano, ninaimani kubwa tuna nafasi ya kushinda ugenini na kwenda kucheza fainali za WAFCON," Shime aliongeza.

Naye nahodha wa Twiga Stars, Oppa Clement, alisema walicheza kwa presha na papara katika kipindi cha kwanza lakini waliporejea walifuata maelekezo ya benchi la ufundi na hatimaye kufunga magoli mawili yaliyowasaidia kujiweka katika nafasi nzuri kwenye kampeni ya kwenda WAFCON.

# Michezo

Jumamosi Desemba 2, 2023

Nipashe




Fati kukaa nje muda mrefu UKURASA 22



Benchikha Gamondi

## Shime: Bahati imetubeba

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), dhidi ya Togo, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, ameweka wazi anaenda kufanyia kazi makosa aliyobaini kwenye kikosi ili kuhakikisha wanafikia malengo.

Togo itaikaribisha Twiga Stars Desemba 5, mwaka huu katika mchezo wa marudiano na mshindi wa jumla atafuzu fainali hizo zitakazofanyika mapema mwakani.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema baada ya kukamilika kwa dakika 90, anafurahi wamepata matokeo mazuri wakiwa nyumbani ambalo ndio lengo la mchezo lakini anakiri nyota wake walikuwa wanafanya makosa ambayo hayatakiwi kujirudia watakapokuwa ugenini.

Shime alisema timu yake haikucheza vizuri sana kutokana na aina ya mchezo wenyewe ambao ulikuwa na presha ya kutaka kushinda na ukubwa wa mpinzani waliyekutana naye.

"Yote kwa yote tumetumia nafasi tatu vizuri kwa kufunga mabao matatu, pamoja na mambo

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba, Yanga fanyeni kweli

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## ●●● Vigogo hao wanahitaji ushindi tu ili kujiweka pazuri makundi CAF...

WAWAKILISHI wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga, zote za Dar es Salaam leo watakuwa dimbani katika viwanja tofauti kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu katika mechi za hatua ya makundi.

**Yanga watashuka nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 1:00 usiku kuwaalika vigogo kutoka Misri, Al Ahly wakati Simba itateremka kuwavaa wenyeji, Jwaneng Galaxy katika mji wa Francistown nchini, Botswana.**

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi ya kwanza dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria huku Wekundu wa Msimbazi ikilazimishwa sare na ASEC Mimosas ya Ivory Coast.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema timu yake imejiandaa vizuri na wachezaji wake walipata muda wa kupumzika baada ya kurejea kutoka kwenye majukumu ya kimataifa.

Gamondi alisema maandalizi waliyofanya kuelekea mchezo huo ni ya kiwango cha juu na kila mchezaji yuko tayari kupambana ili kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo wa nyumbani na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Wachezaji wana morali kubwa kuelekea mchezo huu, Al Ahly ni timu kubwa Afrika lakini tunaenda kucheza tukiwa 11 na wao 11, hivyo tutakutana nao uso kwa uso, kila kitu kinawezakana ndani ya dakika 90.

Tulipoteza mechi nchini Algeria, tukarudi nyumbani na kufanyia kazi madhaifu yetu, sasa tunaenda kukutana na timu yenye falsafa ya timu ambayo tumetoka kucheza nao (CR Belouizdad), lakini muda huu haturuhusu kufanya makosa yaliyojitokeza awali," alisema Gamondi.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema wachezaji wamejipanga vizuri na wamesahau matokeo yaliyopita na sasa wanampango mzuri wa kutafuta ushindi nyumbani.

Mwamnyeto alisema wamejipanga kutoruhusu mabao baada ya kuangalia ubora wa safu ya ushambuliaji ya wapinzani na kazi iliyobakia ni kwa viungo wa na washambuliaji wao kutekeleza majukumu yao.

"Tumejipanga vizuri na tuko tayari kukutana na Al Ahly, tunatambua utakuwa mchezo mgumu lakini tumedhamiria kupambana kutafuta ushindi katika mchezo wetu wa nyumbani," alisema Mwamnyeto.

Kocha Mkuu wa Al Ahly, Marcel Koller, alisema kikosi chake kiko tayari kucheza mechi hiyo ambayo itakuwa ngumu kutokana na matokeo ya mechi iliyopita ambayo wenyeji wao walifungwa.

Koller alisema haangalia historia ya Yanga na kwake kikubwa anaangalia mechi iliyopo mbele yao na maandalizi waliyofanya ya kutafuta pointi tatu na kuzingatia wanacheza ugenini.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji matokeo, hatukuwa na matokeo mazuri ndani ya uwanja huu lakini kila siku kuna vitu vipya, tumefanya maandalizi kulingana na mechi tutakayocheza, tumejipanga kuhakikisha tunashinda katika mchezo wetu wa kesho (leo)," alisema Koller.

Ikifika salama Botswana, Simba imesema iko tayari na kamili kuelekea mechi ya raundi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Af-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >